
NOVEMBA MMXXV - TOLEO LA XLVIII

# NGURUMO

*ya Mwandishi*




## VITABU NI HIFADHI

*ya maarifa na utamaduni*

**HABARI KUU:**

- MAONESHO YA 32 YA VITABU TANZANIA
- Mjue AGORO ANDURU

## YALIYOMO

**TAHARIRI— Uk 02**
VITABU NI HIFA DHI YA MAARIFA...

**MWANDISHI WETU— Uk 03**
ELIAS SHELUKINDO

**NEW IN TOWN: Uk 04**
KOSA LA SIRI na SINTOKUSAHAU MILELE

**PITIO LA VITABU— Uk 05**
CHUNGU TAMU—3

**SAIKOLOJIA: Uk 06— 07**
ISHI KULINGANA NA ISHARA ZA KISAIKOLOJIA UPATAZO (2)

**MAKALA: Uk 08 - 09**
KITABU HIKI WAPASWA KUWA NACHO (marudio)

**KUTOKA KWA FANANI: Uk 10**
KAMBA ZA FRANK MASAI (2)

**SAKO KWA BAKO – Uk 11**
Ameandika MERVAT SAKR

**RIWAYA: Uk 12—13**
MSALITI '10'

**RIWAYA: Uk 14—15**
Najutia Kuwa Na Wewe '10'

**YA KALE NI DHAHABU: Uk 16**
SAFARI 7 ZA SINDBAD BAHARIA

**HABARI MOTO: Uk 17**
MAONESHO YA 32 YA VITABU

**SHUBAKA LA VITABU: Uk 18**
MAAJABU YA USOMAJI WA VITABU

**KITABU NILICHOSOMA: Uk 19**
MENO YA MBWA

**MATANGAZO: Uk 22**

**MALENGA WA KILEO: Uk 21**
TANZANIA MAMA YETU na HUYU NI WANGU AYUNI

**HABARI PICHA: Uk 20**

**KUTOKA MAKTABA: Uk 23**

**ELIMU JAMII: Uk 24 & 25**
SAFARI YA MALEZI (6): MITINDO YA MALEZI

**HADITHI: Uk 26 - 27**
Happy New Year '12'

**HADITHI: Uk 28 - 29**
NGUVU YA KIAPO '07'

## TAHARIRI:

### VITABU NI HIFADHI YA MAARIFA NA UTAMADUNI

Salaam kwenu nyote,

Karibuni katika toleo letu la 48. Ninayo furaha kubwa sana kukuambieni kuwa sasa tumefunga miaka mine na tunauanza mwaka wa TANO. Hakika NGURUMO YA MWANDISHI imefanikiwa kuunguruma vyema ndani na nje ya mipaka ya Tanzania na Afrika.

Tutaandika makala maalum katika toleo lijalo ili kukusimulia safari nzima ya Ngurumo hili.

Mwezi wa Novemba ulibeba tukio kubwa sana la maonesho ya vitabu ya 32 hapa Tanzania. Maonesho yaliyofanyika pale Maktaba Kuu ya Taifa, Upanga, Jijini Dar es salaam.

Kwakweli kama kuna kitu kilinifurahisha katika maonesho haya haikuwa uzuri wa mabanda wala mipangilio ya vitabu kwenye rafu za mashubaka bali wazazi walivyokuwa wakija na watoto wao. Mzazi mmoja alikiri wazi kuwa ametumia zaidi ya shilingi 50,000 kumnunulia mwanawe vitabu.

Ndiyo, vitabu ni hifadhi ya maarifa na utamaduni. Kwa kusoma vitabu tutapata na tutaifadhi maarifa anuai alikadhalika tutalinda na kutunza utamaduni wetu. Watoto wayajifunza maadili mema, tamaduni na desturi za maisha yetu kama tutawanunulia vitabu vya Kitanzania.

Lakini jingine ni kwamba niligundua kuwa kelele tunazopiga kila kukicha kuwa wazazi wabadilike na kuwanunulia watoto wao vitabu zinawafikia taratibu. Watoto walijitokeza sana wakiwa chini ya wazazi wao na kujipatia nafasi za kusoma na kununu vitabu.

Sisi kama Ngurumo, tunawapongeza PATA lakini pia tunawaomba kwa maonesho mengine kuboresha zaidi na zaidi ili tupate watoto wengi na vijana wa kutosha. Kuwa na hata machapisho ya bure ambayo wataondoka nayo majumbani mwao.

Basi, niwatakie Disemba njema! Heri kwenu kwa Krismas na Mwaka mpya! Tuonane 2026 Mungu akipenda tusherehekee mwaka wa TANO wa Ngurumo ya Mwandishi!

**NGURUMO YA MWANDISHI**

**WASILIANA NASI**
**0766 974 865 AU 0627160016**
**WhatsApp: +255 766974865**

## MWANDISHI WETU:
## ELIAS SHELUKINDO

www.richardmwambe.com JAMVI la SIMULIZI

**Tukiwa tunamalizia mwaka wa 4 wa Ngurumo ya Mwandishi, pia tunamalizia marudio ya waandishi wetu.**

**Katika toleo hili tunamrudia Elias Shelukindo, karibu umjue vyema mwandishi huyu kindakindaki.**



Naam, naitwa Elias Shelukindo.
Ukimzungumzia Elias ni kijana kutoka Kaskazini mwa Tanzania, huko Manyara. Upande wa elimu ya msingi na sekondari zote nimezipata hukohuko Manyara. Upande wa familia ni mzaliwa wa pili. Kwa sasa nipo Dodoma nikimalizia elimu yangu ya diploma katika chuo cha elimu ya biashara (CBE).

Kwenye upande wa uandishi, kiukweli ni kitu ambacho nilijikuta tu nataka kukifanya, hamu na shahuku ya kuwa mwandishi wa riwaya viliniteka. Nashukuru Mungu sikuwa mgumu, nikakubali kutekwa na sasa nipo ndani ya maisha ya uandishi.
Kwa ufupi sana, nakumbuka kipindi flani nikiwa shule ya msingi nilikuwa msimuliaji mzuri sana wa hadithi za kutunga mwenyewe na nilipofika sekondari nikaendelea na usimuliaji na wakati flani nikiwa bado sekondari nikapata wazo la kuandika katika daftari hadithi zangu.

Nashukuru Mungu wanafunzi wenzangu waliopata nafasi ya kusoma madaftari yangu ya hadithi walipokea vizuri sana. Hapo nikapata nguvu ya kuendelea kufanya. Nafikiri ni msukumo kutoka ndani ndio ulinitelekeza katika hii dunia ya uandishi.
Nilipomaliza elimu ya sekondari mwaka 2019, nikaanza kupekua mitandao ya kijamii, lengo ni kusoma kazi za waandishi waliopo katika hiyo mitandao. Nilibahatika kukutana na kazi za ndugu yangu, Abyas Mzigua. Alinivutia namna anavyoandika, baadae nikapata nafasi tena ya kupita katika darasa lake. Hapo nikapata maarifa mengine tofauti na ya asili niliyokuwa nayo. Rasmi na mimi mwaka huo nikaanza kuchapa kazi zangu Facebook japo sio sana.

Mpaka sasa Shelukindo nimeandika vitabu vingi tu, ila ambavyo vipo kwa jina langu ni vitabu vitano ambayo ni rasmi na ambavyo vipo tayari kwa wasomaji wa riwaya za kitanzania. Nasema nimeandika vingi bila ya kutaja idadi sababu hivyo nilivyo vipa jina la vingi nimendika kwa niaba ya waandishi wengine maana pia mimi ni Ghost Writer.


Mpaka sasa nimebahatika kuchapa vitabu vitatu. Ambavyo ni;
-Kwaya ya Jasusi,
-Kikao Kabla ya Mazishi na
-Msemaji.
Changamoto ni muda, ukizingatia nipo kwenye masomo ambayo yanatumia muda mwingi darasani. Upande mwingine ni fedha kwa ajili ya kuchapa vitabu kwa ajili ya wasomaji wangu. Hivyo tu.

Kwanza kila mwandishi wa riwaya ni rafiki kwangu, kusema ukweli tu, nikijua wewe ni mwandishi basi moja kwa moja nakufanya rafiki. Kwenye ishu ya waandishi wanao nivutia kwanza kuna Abyas Mzigua, sababu ambazo kwenye historia yangu nimeziweka wazi. Halafu kuna George Iron Mosenya, namna anavyotunga visa vyake kipeke yake. Mwingine ni Japhet Nyang'oro, namna anavyopanga matukio katika riwaya zake. Kwa kweli wapo wengi sana ila acha nimalizie na Crarency Sanga, ananivutia namna anavyokazana sana kwenye dunia ya uandishi.

Soko la vitabu limekuwa gumu? Mimi nijibu swali hili kwa maneno machache tu. Waandishi tuache kusukuma kazi za fasihi kwa kujuana na makundi. Huku kujuana na makundi ni moja ya sababu soko linakuwa gumu. Hivyo tu.
Kwanza mtu akitaka kupata kazi zangu, njia rahisi ni kuwasiliana na mimi kwa namba 0765391580. Kwenye mitandao ya kijamii nipo Facebook, andika HADITHI ZA SHELUKINDO na SHELUKINDO WA HADITHI utakuwa umemaliza.

Neno langu kwa wapenzi wa fasihi, wasiache ama kuchoka kusoma riwaya za Kitanzania maana ni za kwao na tunaandika kwa ajili yao, pia kwa wapenzi wa riwaya hizi kama una uwezo wa kifedha usisite kuwekeza kwa mwandishi yeyote unayehisi unaweza kumsaidia. Hasa waandishi wachanga.
Asante. E.S


## NEW IN TOWN :
## SITAKUSAHAU MILELE na KOSA LA SIRI




AMBOKILE ni kijana mahiri kutoka kijijini. Anaingia jijini Dar es salaam kwa ajili ya kujitafutia maisha bora kutokana na kutingwa na ugumua wa maisha uliopo kijijini. Anafika jijini na jiji linampokea, maisha yanaanza kubadilika pale anapoamua kuweka uvivu pembeni na kuanza kupambana ili kuweza kuusaka mkate wake wa kila siku.

Katika harakati hizo anakutana na mwanamke wa ndoto zake, Ashura ambaye anakuwa mwandani wake na kumpatia zawadi njema ya uzao. Lakini hapo katikati kidudu mtu anaingia na kuisambaratisha familia ile. Je kidudu mtu hicho ni kipi na vipi Ambokile ataweza kuyashinda yote na kuiridisha familia yake mikononi mwake?
Ungana na Gabriel Shewio akisema “nilidhani nimepata, kumbe nimepatikana!”

**Kitabu kinapatikana Duka letu la Kona ya Riwaya Kinondoni!**




**Mwandishi: Ben Mkota**

“… kuna new twist ama sijui niite new development katika kesi yako. Amejitokeza mama fulani na kukiri kwamba ndiye aliyehusika na kwamba alikusingizia tu kosa lile… kwa hivyo, waziri ametoa agizo uachiliwe huru with immediate effect!”

Auni anaupata tena uhuru wake baada ya kutumikia kifungo jela kwa takribani miaka thelathini kwa kosa ambalo inavyokuja kubainika, hakulifanya. Badala ya kuufurahia uhuru ule, moyo wake unaumia zaidi kwa ufichuzi kwamba kuhukumiwa na kufungwa kwake kulikuwa kosa, na kulimfanya apoteze kila alichokithamini maishani. Sababu inayotolewa ya kumweka huru vilevile inamwacha na maswali mengi kuliko majibu.

Je ni nani huyo aliyemsingizia kosa lile? Kwanini alimsingizia kosa hilo? Kumsingizia kosa hilo kulilenga kuficha siri gani?

**Jikamatie nakala yako sasa kwa Tsh 10,000 tu.**

# Diwani - CHUNGU TAMU (3)



**DIWANI YA CHUNGU TAMU**

**MWANDISHI: THEOBALD MVUNGI**

**WACHAPISHAJI: TPH**

**MWAKA: 1985**

**Inatoka toleo lililopita…**

Katika shairi la **"Daktari Askari"**, mwandishi anaonesha jinsi waganga wanavyojua umuhimu wa kuwajibika katika kazi yao ya utabibu. Ameonesha kuwa wale waganga waliwahudumia majeruhi kwa bidii wakati wa vita. Hivyo kila mtu anatakiwa kuwajibika kama wale waganga ndipo tutaweza kulisukuma mbele gurudumu letu la ujenzi wa jamii endelevu.

Katika shairi la **"Chanzo ni Wenye Kauli"** mwandishi anaonesha utekelezaji na uwajibikaji mbovu unavyosababisha rushwa, magendo na ulanguzi katika jamii yetu. Katika shairi hili mwandishi ameonesha dhahiri kuwa uzembe toka kwenye vyombo vya dola ndio umechangia uwajibikaji kuwa mbovu.Mwandishi anasema;

*"Chombo hiki kuzembea,*

*Chanzo kilichozidia,*

*Magendo kuyatetea,*

*Watu kuwasaidia,*

*Chombo kilididimia."*

Katika shairi la **"Wimbo Wake Hotubani"** mwandishi anaonesha utekelezaji mbaya wa maazimio unavyochangia kuzorota kwa maendeleo ya jamii yetu. Katika shairi hili, mwandishi ameonesha kuwa viongozi wetu wametuna ofisini na shambani hawaingii, wanatumia madaraka vibaya, maagizo ni midomoni bila utekelezaji, kila siku-mchana kutwa wanakunywa na kulewa, n.k. Utekeleaji wao uko kwenye hotuba, Mwandishi anasema;

*"Cheo kiko mkononi,*

*Agizo li mdomoni,*

*Mchana kutwa ndotoni,*

*Wimbo wake hotubani,*

*Raia kazi fanyeni."*

Katika shiri la "**Wengine Wabaki Taabuni"**, mwandishi anaonesha jinsi uzembe kazini, kutowajibika ipasavyo, usaliti pamoja na rushwa unavyorudisha nyuma utekelezaji mzuri wa maazimio tunayojiwekea. Mwandishi anaitaka jamii ifahamu na kutambua umuhimu wa kazi na wajibu wa kila mmoja katika jamii ndipo tutaweza kufanikisha kuijenga jamii mpya.

### 3. UONGOZI MBAYA


Suala la uongozi mbaya limekuwa tatizo sugu kwa nchi nyingi za Afrika. Waandishi wengi wameonesha jinsi ambavyo viongozi wengi walioshika madaraka baada ya mkoloni kuondoka walivyotekanyara uhuru uliopatikana, kwa hiyo mabadiliko yakawa rangi ya ngozi tu, kwani wananchi wengi waliendelea kuteseka katika umasikini wao. Katika shairi la "**Tishio la Binadamu"** mwandishi anasema;

*Mashindano ya silaha, yamekuwa ni mchezo,*

*Wakubwa waona raha, kwa silaha waundazo,*

*Mabomu yaso na siha, ndiyo yawapa uwezo,*

*Urusi na Marikani, dunia mwaipa adha.*




www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Mwandishi anakemea juu ya uongozi unaotumia mabavu. Mfano mzuri mwandishi anakemea nchi za Urusi na Marekani ambazo ni wanachama wenye kura ya VETO kwenye umoja wa Mataifa zinavyotumia mabavu kuzikandamiza nchi zisizo na nguvu kisilaha. Mwandishi anasema;-

*"Kuyasujudu mabavu, mwadai tusilotaka,*

*Maoni yetu chakavu, sawa nguo ya miaka,*

*Ni pengi penye makovu, nchi zilivyopasuka,*

*Mabomu yateketeza, waundaji mwafurahi!"*

***Itaendelea toleo lijalo...***

# -SAIKOLOJIA-

## ISHI KULINGANA NA ISHARA ZA KISAIKOLOJIA UPATAZO - 2 -



**ISHI KULINGANA NA ISHARA ZA KISAIKOLOJIA UZIPATAZO.. [PART 2]**

Ni makala ya kisaikolojia tena kwa mwezi NOVEMBA. Sina shaka u bukheri wa afya tele. Ikiwa unapitia changamoto yoyote ya kiafya au ya kisaikolojia nikusihi sana utumie nguvu yako ya asili katika kufanya mambo yaende au idhinisha mambo yaweze kutokea au yasitokee.

Nakuusia na najiusia na mimi, ni mwishoni kabisa mwa mwaka, sio mbaya ukalipa ada hivi sasa, sio mbaya ukanunua mavazi ya sikukuu hivi sasa. Sio mbaya ukinunua mahitaji ya vyakula vya sikukuu hivi sasa. Ni watu wanaoishi kwa mipangilio ndio wanaoonekanaga kuwa ni watu wanaojiweza kumbe ni ile hali ya kupangilia vizuri mambo yao. Ukitaka usichanganyikiwe Kisaikolojia basi ishi kwa kupangilia vizuri mipango yako. USIOGOPE KUONEKANA WA KIZAMANI, AU KUONEKANA MWOGA WA MAISHA. ISHI UKIJIPANGILIA KUIISHI LEO NA KUPANGILIA KESHO NA KESHO KUTWA.

Katika toleo hili tunaangazia sehemu ya pili ya mada iliyopita iitwayo ISHI KULINGANA NA ISHARA ZA KISAIKOLOJIA UZIPATAZO, ambapo tuliona njia mbalimbali ambazo Mungu huzitumia kumwasilishia mwanadamu ishara mbalimbali ambazo humpa taarifa au tahadhari katika maisha yake ya kawaida, mfano wa ishara hizo tuliona ni kama mikono kuwasha kuwa ni ishara ya kupata pesa, mdomo kucheza kuwa ni ishara ya kugombana na tukaona pia wapo wanaopata ishara katika ndoto waotazo.

Katika toleo hili tuangazie ni namna gani unaweza kutumia nguvu ya asili katika kufanya ishara hizo zikatendeka au zisitendeke.

**TAFUTA MAHALI TULIVU, TULIA**

Maandalizi ya kutumia nguvu za asili yanatakiwa kufanyika, andaa mahali pa utulivu, tulia ukiwa umesafisha mwili wako. Jifanyie usafi wa kutosha na mahali hapo utakapoandaa ili kuwa katika utulivu napo pawe katika hali ya usafi. Fikra zako zisiwe katika mawazo ila tu zinaweza kulibeba hilo jambo ambalo unataka kulishughulikia kisaikolojia. Pata utulivu ukiwa umejituliza katika ukimya ili kuruhusu mabadiliko na nguvu ya asili kutokea.

**AMSHA NGUVU YAKO**

Uwe mahali peke yako, ukihakikisha pako na utulivu wa kutosha. Amsha nguvu iliyopo ndani mwako. Amsha asili ya uumbaji na mawasiliano ya ndani yanayohusisha roho yako na Mungu wako. Hakikisha hautulii hadi uyasikilize mabishano au makubaliano ya nafsi mbili ndani ya moyo wako. Hakikisha moyoni mnakua wawili huku kiuhalisia upo peke yako.

**TAMKA ITOKEE NDANI YA MOYO WAKO**

Kile ulichopata ishara yake, kama ni mkono wa kulia umewasha ambapo kwako ni ishara ya kupata pesa ila inapitiliza, basi tamka kuwa pesa ipatikane na pia itulie. Mdomo wa chini unakucheza,wakati kwako ni ishara ya kugombana basi tamka matamshi ya kukataa ugomvi.
Unapotamka kuidhinisha jambo au kukataa jambo lile litokee au lisitokee hakikisha unatamka kwa nguvu kuu kutoka ndani ya moyo wako kiasi cha kuruhusu nguvu yako ya asili kuliumba jambo hilo. Hakikisha ndani ya moyo wako jambo au utamkwaji huo umetimilika.

**HAMISHIA VYA MOYONI KUWA UHALISIA**

Umeshatoa nguvu kimatamshi, sasa hamisha nguvu ile kutoka moyoni kuja katika uhalisia. Hakikisha unaachilia kwa nguvu unachokiona moyoni ukione usoni pako. Ione ile nguvu kiuhalisia.

**PALILIA NA MWAGILIA HADI JAMBO LITOKEE**

Umeshalileta llile jambo usoni mwako, hakikisha unalipalilia jambo hilo mpaka linatokea. Lipalilie jambo hilo kwa kufanya



## ISHI KULINGANA NA ISHARA ZA KISAIKOLOJIA UPATAZO - 2 -

matendo mema, hapa nguvu zako za asili zina uhusiano kabisa na usafi wa moyo wako, yaani moyo wako usiwe katika kujihukumu au kuhukumiwa kwa jambo lolote.

**AMINI IMETOKEA**

Moyo wako ukishakua msafi katika kufanya jambo litokee, unalipalilia jambo hilo kila wakati kwa maombi kulingana na imani ya dini yako, amini jambo limetokea. Pasipo Imani, elimu yote hii ni bure.

**MSHUKURU MUNGU**

Nani asiyemjua Mungu? Nani asiyejua kuwa Mungu ndio muweza wa kila kitu? Hata wanasaikolojia na wanasayansi wanapofikia mahali ambapo akili za ndani na nje hugota au kufika mwisho huwa wanautambua uwepo wa Mungu katika maisha ya mwanadamu. Ili mambo yatokee basi huna budi na ni muhimu kumshukuru Mungu. Mshukuru Mungu ili mambo yatokee katika uhalisia.

Nikutakie mema na mafanikio katika kuyaishi yale Mungu anayokuonyesha.

Ikiwa utahitaji ushauri na mtu wa kuzungumza nae ili kupata ushauri wa kisaikolojia katika jambo lolote basi wasiliana name kupitia +255763013206.

MADAM NEEMA MGAO.
DODOMA.
TANZANIA.




## KITABU MARKET

Tovuti mpya ya KITABU MARKET imekuwa hewani karibu mwezi mmoja sasa.

Katika tovuti hii, utapata vitabu vya hadithi, maarifa, makala mbalimbali na majarida ya Ngurumo.

Tovuti hii imegawanya  maudhui yake katika makundi manne.

1. KITABU CHA BURE
Katika safu ya Kitabu cha Bure msomaji ataweza kusoma vitabu na majarida na machapisho mengine bure kabisa.

2. MAKTABA
Katika safu ya Maktaba, msomaji atatakiwa kujiunga na uanachama wa Maktaba ndani ya Tovuti hii kwa malipo yatakayopendekezwa. Ndani ya MAKTABA utaweza kusoma vitabu vya aina mbalimbali kadiri ya uwezo wako. Msomaji akilipia ataweza kusoma machapisho hayo katika mfumo wa pdf pasipo kupakua katika simu yake.

3. NUNUA KITABU
Katika safu ya Nunua Kitabu, msomaji ataweza kununua kitabu kwa bei itayoelekezwa katika tovuti. Akishanunua ataweza kukipakua na kukisoma kwa wakati wowote katika simu yake hata akiwa hana bando.

4. JARIDA LA NGURUMO
Katika safu hii utasoma matoleo yote ya jarida la Ngurumo ya Mwandishi kuanzia 1 mpaka 48 ambapo tupo sasa.

Anza sasa kuperuzi tovuti hii kisha utupe maoni yako.

Tembelea sasa tovuti yetu.

https://kitabumarket.co.tz/

Mjuze na mwenzio!

MJUE MWANADAMU NA NGUVU ZILIZOMO NDANI YAKE

Ni kwa 15,000/= tu. *(Marudio)*

**MJUE MWANADAMU NA NGUVU ZILIZOMO NDANI YAKE**

**ISBN: 9789912429321**
**COSOTA: C0868882**

BEI YA NAKALA HALISI TSH 15,000/= au kodisha kupitia online. Link na mawasiliano yapo chini

Katika safari ya maisha, mwanadamu hujikuta akitafuta majibu ya maswali ya ndani kuhusu asili yake, uwezo wake, na nafasi yake katika ulimwengu. Kitabu hiki si tu muongozo wa kiroho, bali ni mwaliko wa kuangalia ndani ya nafsi, kugundua hazina iliyofichika na kuishi maisha yenye kusudio. Ni matumaini yangu kuwa kila ukurasa utakuwa mwanga mpya katika safari yako ya kiroho.

**MAWAZO NA HISIA**

Kwenye kurasa hizi utajifunza na kuelewa kwa kina jinsi mawazo yanavyoweza kuleta athari kubwa kwenye maisha yako. Utagundua kuwa kila kitu kinachoonekana chanzo chake ni mawazo na fikira tu. Lakini utaelewa kwa kina kuwa hisia zako ni sawa sawa na shamba lenye rutuba nzuri, hivyo linaweza kuotesha aina yoyote ya mbegu na kuvunwa kama mavuno bora. Hivyo, kile kinachoitwa hisia za huzuni au furaha ni matokeo ya mawazo yako mwenyewe. Hakuna anayeweza kukufundisha wewe kuwa na hisia nzuri, na hatimaye utagundua kuwa matendo yako ni matokeo tu ya mawazo na hisia zako.

**SIRI ZA NISHATI**

Katika sura ya pili, utajifunza na kuelewa kinaga ubaga kuhusu nguvu au nishati inavyoingia na kuanza kufanya kazi mwilini mwako. Sasa utaelewa kwa kina kuhusu miujiza na maajabu ya mwanadamu kuumba na kutengeneza dunia kupitia macho na moyo wake. Chakra ni vituo vya nishati; vituo hivi vinatumika kupokea na kusambaza nishati (prana). Binadamu ana vituo saba vya nishati, kuanzia root chakra mpaka crown chakra. Lakini pia binadamu ndani na nje ya mwili huu wa nyama ana miili sita mikubwa ambayo yenyewe ipo katika mfumo wa mwanga (subtle body). Hii ndiyo inasaidia kulisha na kutunza mwili wa nyama.

**KANUNI ZA MAUMBILE**

Utaendelea kusoma na kujifunza zaidi. Utajifunza kanuni za Mungu ambazo zinaongoza vitu na maumbo yote, ikiwemo maji, udongo, mimea, hewa, moto, na kila kitu. Hapa utajifunza kwa kina kanuni kama vile: kanuni ya umoja, kanuni ya chanzo na matokeo, kanuni ya mvuto, kanuni ya _kuwa-tenda-pata_, kanuni ya uwili, kanuni ya jinsia, na kadhalika.

Sasa utakua dereva mahiri ambaye anajua taratibu na sheria za barabarani. Sasa utaweza kuendesha maisha yako katika mwanga bora sana, kwa kuwa sasa utakuwa unafahamu kwamba kila kitu katika ulimwengu huu ni wewe mwenyewe. Chochote unachokifanya haufanyi kwa faida ya wengine bali kwa faida yako, kwa kuwa kila unachokiona ni taswira *(reflection)* ya wewe mwenyewe. Utagundua maisha ni kioo.

Utagundua kuwa kwenye maisha ni kuchagua muda na nafasi, kwa kuwa maisha ni mchezo mtakatifu unaotumia akili, hisia, na matendo.

**MAISHA NJE YA MWILI (ASTRAL TRAVEL)**

Utasoma mada za kutoka nje ya mwili, ndoto, na uchawi. Utajifunza jinsi ambavyo nishati inavyosafiri na kubadilisha maumbo kwa kutumia hiyo miili yako ya nje. Utaweza kugundua kuwa kumbe kinachotoka nje usiku ukiwa umelala huwa ni huo mwili wako wa tatu (astral body and astral travel). Na kitendo hicho si uchawi au maajabu kama ulivyoambiwa au kusikia, bali ni takwa la msingi sana la kimaumbile kama ilivyo kuingiza pumzi na kutoa pumzi nje. Kwa kuwa kitendo cha kupumua ni kitendo cha kiroho pia. Kupitia astral travel utakuja kugundua ugunduzi wote wa kisayansi na kitaaluma ulifanyika kupitia ndoto, na hicho kinachokuwa kinaota ni mwili wako wa tatu.

**MAPENZI NA NDOA**

Hapa utajifunza kwa kina na kuelewa siri za uumbaji wa ulimwengu ambazo asili yake ni tendo la ndoa. Kumbe nguvu ya sacral chakra ndiyo asili ya kila kitu.

Hapo utajua nguvu ya tendo la kujamiana katika kuleta mafanikio, utajiri, au kuleta uharibifu kwenye maisha yako. Utakuja kujifunza namna nzuri ya kuitumia nguvu hii katika ustawi wa maisha yako na jamii yako.

Utaweza kuwa mwangalifu sana kwenye kufanya mapenzi (sacred energy exchange/sex). Sio kitendo cha kiakili bali ni kitendo kitakatifu. Hauwezi tena kufanya sex kwa kujaribu au kwa sifa, kwa kuwa sasa unaelewa ni nini kilichomo ndani yake.

**TAHAJUDI (*MEDITATION)***

Kwenye sura ya mwisho utajifunza tahajudi (meditation). Kwa kuwa sasa umeshajitambua wewe ni nani, hakika sasa wewe ni dereva mahiri. Dereva ambaye sasa unaweza kwenda kusoma mara kwa mara kupata ujuzi zaidi.

Meditation kwa lugha rahisi ni muunganiko wa nafsi yako na Muumba wako, kama ambavyo Yesu alisema "Mimi na Baba ni kitu kimoja," au kama ilivyo mbinguni na duniani. Imekuwa unapofanya meditation unawasiliana moja kwa moja na Muumba wako na hivyo kupata maarifa makubwa na busara za uumbaji moja kwa moja wewe mwenyewe, kwa kuwa wewe ni sehemu ya huo uumbaji.

Hapo utajifunza aina nyingi sana za meditation. Utaweza kujifunza meditation maalumu kwa ajili ya uchumi na fedha, meditation maalumu kwa ajili ya afya, meditation maalumu kwa ajili ya masomo, meditation maalumu kwa ajili ya ulinzi wa kiroho, meditation maalumu kwa ajili ya mahusiano, na kadhalika.

Nakualika tena usome kitabu hiki. Ni zaidi ya kitabu, hii ni njia ndogo inayomulika moyo wako na kukuongoza kwenye safari ya maisha.

**Bookshop na mawakala mbalimbali**

1. Elite book shops
Mbezi beach: 0753435484
2. University of dar es salaam: 0658780015

3. Palm village: 0767861151
4. Shoppers plaza: 076786151
5. Dodoma : 0745199860
6. Moshi Kilimanjaro: 0768954365
7. Tph Book Shop Mtaa wa Samora Posta: 0742556446
8. Kahama Shinyanga Phone: +255754056968
9. Kigoma Phone: +255620482945

Au wasiliana na mwandishi mwenyewe Chelestino Malinga 0754062900/ 0655062900. Pia waweza Soma online kupitia link hii hapa chini

https://lantern.co.tz/books/mjue-mwanadamu-nguvu-zilizomo-ndani-yake-9789912429321



## Kamba Za Frank Masai : Sehemu ya 2

*Inatoka katika toleo lililopita…*

**Nazi ngumu ukivunja kwa ugoko tu, ikikutana na nondo inatii amri. Hii imani ilinipa ujasiri mkubwa na ushawishi wa kumtokea yule dada. Nilijua itakuwa tight kumpata lakini kwa maneno yangu, mtoto hatoboi hata dakika 1, atakuwa kaingia kwa Master Gamond. Atabweka mbona.**

Endelea…

Safari ikiwa inaendelea, tukakutanisha macho kwa mara nyingine. Mwanadada akanitazama kwa macho yake ya mafua. Mie moyo unapwita kwa nguvu hadi koti langu linanyanyuka. Hapo tunaingia Kimara Baruti ujue. Tukatazamana kwa sekunde kadhaa afu pisi ikageukia pembeni huku inamumusa midomo. Ikaniua mazima. Hisia zikaenda mbali, maili mbili karibu. Nika*wish* ile midomo ndo iwe ulimi wangu afu amumuse vile. Bwege mimi!

Dakika moja mbele, akageuka tena. Akanikuta bado namtazama. Sasa niliona hata naye uvumilivu umemshinda. Maana akawa hatulii, anajipapasa na kupekua mifuko ya suruali yake bila sababu na mwishowe alivunja ukimya.

"Kaka habari..." Ile sauti kudadex, kinanda si kinanda wala kasuku si kasuku. Naweza kufananisha labda na nyuzi za gitaa la Diblo Dibala. Sauti nyembembe na tamu bila hata kuionja.

"Nambie dada..." Niliitika huku natabasamu kishababi bila kuonyesha meno.

"Vipi..." Aliniuliza lakini hakumaliza kauli yake lakini alitazama mkoba wangu. Sikuelewa

"Safi! Vipi?" Na mie nikajibu na kusalimia.

"Hamna. Nasema vipi huanzi kutangaza sabuni zako na zile dawa za kupaka kupunguza mafua?" Babake nilichoka kuanzia nyonga, miguu mpaka kucha.

Halafu bora angeuliza kwa sauti ya chini, yaani kauliza daladala zima wakasikia. Kulia nashindwa, kukataa nashindwa, kucheka sitaki. Chill imeingia pilipili.

"Kaka!" Aliniita baada ya kuona butwaa langu.

"Konda shusha hapo Maji..." Hii kauli niliitoa kwa sauti ya kibabe na angejitia kunitania ningemkata bonge la kofi. Nilishukia palepale na sikutaka kujua mule ndani walinitazama au walizingatia mitikasi yao.

Lakini kwa kweli niliathirika kisaikolojia. Mie nimeona nimevunja kabati kabisa, kumbe wengine wananiona kama muuza dawa za mafua na sabuni za asili. Kubabeki.

Nikavua koti, nikanunua mfuko nikaweka humo. Nikachomoa shati nilimochomekea, nikalikunja mikono kisha nikatoka lile eneo nadundika kama muhuni. Sikutaka tena kunyata. Safari ya miguu hadi Njia Panda ya Chuo. Pale uhakika kupata ngoma za Makumbusho.

Ila yule dada wala sikuwa naye na nia. Ni shetani tu. Kwanza hakupendeza hata hivyo.

FRANK MASAI katika pozi kupiga watu 'kamba'.



# SAKO KWA BAKO:

**Ameandika mervat sakr**

## Jukwaa la Nasser la Kimataifa lasherehekea Kutambulishwa kwa Kiswahili Kama Lugha Rasmi ya UNESCO

Jukwaa la Nasser limepokea Kwa furaha tangazo la Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) la kuitambulisha rasmi Kiswahili kuwa mojawapo ya lugha rasmi za kazi katika mikutano yake mikubwa. Hatua hiyo imefikiwa wakati wa Kikao cha 43 cha Bunge Kuu kilichofanyika Samarkand – Uzbekistan kuanzia Oktoba 30 hadi Novemba 13, 2025.

Uamuzi huu wa kihistoria ulitokana na ombi lililotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa ushirikiano na Baraza la Kiswahili Tanzania BAKITA na Balaza la Kiswahili Zanzibar BAKIZA, ambapo Balozi wa Tanzania nchini Ufaransa na Mwakilishi wa Kudumu kwa UNESCO, Ali Jaberi Madini, alitoa hotuba ya nchi baada ya uamuzi huo kutangazwa rasmi.

Jukwaa hilo limebainisha katika taarifa yake kwamba kwa mafanikio haya, Kiswahili inakuwa lugha ya kwanza asilia ya Kiafrika kupata hadhi ya lugha rasmi ya kikazi katika UNESCO, jambo linalowakilisha hatua muhimu katika safari ya kutambuliwa kimataifa kwa lugha za Kiafrika na kuimarisha uwepo wake katika mashirika ya kimataifa. Ni muhimu kujua kwamba, tangu Novemba 2021 UNESCO ilikwishaitangaza Siku ya Kimataifa ya Lugha ya Kiswahili, inayosherehekewa tarehe Julai 7 kila mwaka, ambayo baadaye Bunge Kuu la Umoja wa Mataifa liliithibitisha rasmi Julai 2024. Hadi leo, Kiswahili ni lugha rasmi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Shirika la Maendeleo ya Nchi za Kusini na Kati mwa Afrika (SADC), Chama cha Wazalishaji wa Almasi wa Afrika (ADPA), na Umoja wa Afrika (AU).



**Bi. Mervat Sakr**

**Mfasiri na Mratibu wa Lugha ya Kiswahili katika Jukwaa la Nasser**

Katika muktadha huo, mtafiti wa Anthropolojia na Mwanzilishi wa Jukwaa la Nasser la Kimataifa, Hassan Ghazaly alisema kuwa jukwaa hilo linaipa lugha ya Kiswahili kipaumbele cha pekee kupitia idara maalumu inayoshughulika na utekelezaji wa programu za mafunzo, miradi ya tafsiri, na mijadala ya vijana, yote ikitekelezwa chini ya mkakati wa kimkakati anaousimamia yeye binafsi, kwa lengo la kuimarisha hadhi ya Kiswahili hapa Misri kama daraja la mawasiliano na wananchi wa Afrika Mashariki ambao nchi zao zina mahusiano ya kimkakati na Misri.

Aidha, aliongeza kuwa Kiswahili leo hii nchini Misri kinachukuliwa kuwa miongoni mwa nyenzo muhimu katika kujenga uelewa wa Wamisri kuhusu masuala ya bara la Afrika kupitia wanafunzi wa lugha hiyo kutoka Misri, ambao wanachukuliwa kuwa daraja la mawasiliano kati ya tamaduni za Kiafrika, jambo linalodhihirisha nafasi yake inayoongezeka katika medani ya kimataifa na kutambuliwa kwake kunakoongezeka kama lugha ya mawasiliano ya kitamaduni na kibinadamu.

Aidha, Mfasiri Mervat Sakr, ambaye ni mratibu wa Lugha ya Kiswahili katika Jukwaa la Nasser, alisema kwamba idara ya Kiswahili kwenye tovuti ya jukwaa hilo inahifadhi zaidi ya makala 1,675 zilizochapishwa, zinazochangia katika kusambaza maarifa na kuimarisha ukaribu wa kitamaduni kati ya watu wa Kiafrika na Kiarabu. Aliongeza kwamba idadi ya wahitimu wa idara ya Kiswahili katika Jukwaa hilo imefikia wanafunzi 250, na kwa dhamira ya kupanua wigo wa ushiriki, Jukwaa hilo limezindua lango la mtandaoni la kupokea makala kwa Kiswahili, linalopatikana kwa wote wanaozungumza au kusoma lugha hiyo na wanaotaka kuchapisha makala na tafiti zao kwenye jukwaa, kupitia barua pepe: Articles@nasserforum.com.

# MSALITI - 10

Na. Richard Mwambe



*Ilipoishia...*

**Gina alikata mitaa, akizunguka huku na kutokea kule. Akapita mtaa huu mpaka ule kule, yote hayo ilikuwa na kutaka kuijua mitaa hiyo. Aliulizia nyanya mara maparachichi. Na vichache alivyoona vinafaa kununuliwa alivinunua. Akatoka eneo lile na kuelekea mahali yalipoegeshwa magari ya kukodi.**

*Endelea...*

"Nipeleke Mayonzi," akamwambia dereva. Lile gari likatiwa moto na kuondoka mahali pale. Mayonzi hapakuwa mbali, ni mwendo wa dakika kumi na nane tu kutoka pale alipokuwa Gina.

"Nikushushe wapi?" yule dereva akauliza. Gina akawaza harakaharaka maana kwanza hakuwa anapajua Mayonzi. Alichofanya ni kufuata maelekezo tu aliyopewa.

"Nishushe kanisani," Gina akajibu maana alijua wazi kuwa kila sehemu lazima kuwe na 'kanisani'.

"Tumefika!" yule dereva akamwambia Gina na kuegesha gari karibu na wigo mkubwa wa Kanisa hilo. Mwanamke huyo akalipia huduma na kumwacha yule dereva aondoke zake. Alipohakikisha kapotea viungani, naye akavuta hatua kuliendea duka kubwa lililokuwa mkabala na Kanisa lile. Muuzaji alikuwa mwanaume wa makamo, kadiri ya miaka sitini hadi sabini hivi.

Ushupavu wa mwili wake ulionesha hakuwa mwanaume mzembe mzembe. Wakasalimiana halafu yule bwana akaduwaa kusubiri nini mwanamke yule mzuri na mrembo anataka kumwambia.

"Samahani, nahitaji kufika nyumbani kwa Bwana Innocent Kabelwa… sijui unapafahamu?" Gina akauliza. Yule bwana hakujibu harakaharaka, akatupa chini macho yake kana kwamba kuna mtu anayemwangalia. Naam! Kulikuwa na mtu mwingine ambaye aliinuka muda uleule na kusimama. Huyu alikuwa mwanamke aliyeshupaa mwiliwe. Sura yake ilibeba kabisa haiba ya Kinyarwanda.

"Huyo mtu alishapotea hapa miaka mingi sana…" yule mwanamke akajibu. Gina akatulia kimya sekunde kadhaa akiwatazama wale watu kwa zamu na kuhisi jambo fulani.

"Nyumbani kwake ni wapi?" akauliza.

"Mtaa wa tatu nyuma, nyumba namba NG 219, lakini sijui kama utakuta mtu…" yule mwanamke akaeleza, "Samahani… wewe ni nani?" akamrudishia swali mgeni wake.

"Sijui nikuelezeje… mimi ni mmoja wa wanawake zake Innocent, natokea Mwanza, ni muda mrefu sijamwona lakini nakumbuka aliwahi kunielekeza kuwa anaishi maeneo haya ya kanisani," Gina akaeleza vya uongo. Ukiwa mpelelezi uongo na ulaghai ni vitu ambavyo ulimi wako unatakiwa kugandamana navyo, ila sijui kwa Mwenyezi vinawekwa fungu gani; dhambi au sehemu ya kazi? Sijui. Gina alishukuru na kujiondoa kwenye lile duka kuelekea kule ambako ameelekezwa. Wale watu pale dukani wakatazamana. Halafu wakapeana kama ishara. Yule mwanamke akavuta droo na kutoa bastola moja iliyosheheni risasi. Aliikagua na kuihakiki, kisha akaipachika kwenye suruali aliyovaa na kuifunika na fulana yake kubwa. Akatoka bila kuaga na kumwacha yule mwanaume mule dukani.

Gina hakwenda moja kwa moja kwenye ile nyumba. Alipita kando kando ya ule mtaa, kwenye viambaza vya nyumba za wakazi wa hapo huku macho yake yakisoma kila anachokiona na kila anayemwona. Kila mwendo wa hatua mia mbili aligeuka nyuma kuhakiki kama kuna mtu anayemfuatilia. Baada ya nyumba kadhaa, alipogeuka, moyo wake ukapiga kwa nguvu kwani alimwona mwanamke yuleyule aliyemwacha kule dukani akiwa kama hatua mia mbili nyuma yake. Mwili wake ukamsisimka akajua kuna hatari. Mambo yameanza kunoga. Akaongeza mwendo na kutembea haraka haraka kufuata ile barabara iliyokuwa na ukimya maana wakazi wake walikuwa gulioni. Zaidi alipishana na wanafunzi na watu wachache wanaohesabika. Alipofika kwenye nyumba moja ambayo iliacha uchochoro kati yake na nyumba nyingine, ambapo hata Toyota Vitz lingeweza kupita, akakunja kona kuelekea ule uchochoro kisha akasimama na kuvua lile kofia.

Gina alitaka kuhakiki kama mwanamke huyo alikuwa akimfuata au alikuwa na *mishemishe* zake. Akachungulia, lakini hakumwona yule mwanamke kule barabarani. Hofu ikamjaa. Akajua wazi kuwa atakuwa kaingia kwenye moja ya njia ambazo angetegemea kukutana naye upande huo wa nyuma. Akatabasamu. Akajipapasa mapajani. Bastola zake zilikuwa zimetulia kimya kabisa zikisubiri amri tu. Basi, akajitokeza tena barabarani na kuendelea na safari

# MSALITI - 10



yake. Akafika hadi kwenye geti la nyumba ile aliyoelekezwa kuwa ndiyo anayoishi Innocent Kabelwa. Naam! Kibandiko kwenye lango la nyumba hiyo kilikuwa na taarifa sawia na zile alizopewa na yule mwanamke kule dukani. Akajaribu kugonga na kugonga lakini hakukuwa na mwitikio wowote. Akatazama bustani ya nyumba ile, nayo ikampa ishara kuwa hakukuwa na kiumbe kinachoishi humo. Alipogeuka nyuma kuondoka, macho yake yakagongana na yule mwanamke aliyekuwa ng'ambo tu ya ile barabara.

"Hukuamini kama nitafika au?" Gina akatupia swali.
"Si hivyo…"
"Ila…" Gina akahoji.
"Ngara hapaaminiki, mume wangu aliniambia nihakikishe usalama wako," yule mwanamke akajibu.
Gina akasimamisha daladala lililokuwa linapita na kujitoma ndani. Akaondoka na kumwacha yule mwanamke palepale. Dakika kama arobaini na tano hivi aliwasili Ngara Super Lodge. Akamkuta Amata akiwa mgahawani kwa chakula cha mchana.
"Umefanikiwa?" Amata akamuuliza Gina. Naye akamsimulia kila kitu na jinsi ilivyokuwa huko alikoenda. Amata akaacha kula na kubaki akimsikiliza.
"Kwanini huyo mwanamke akufuatilie?" akauliza.
"Sijui!"
"Basi…" Amata akasema huku akigongagonga vidole vyake mezani. "Huyo mwanamke na huyo mumewe wanajua jambo kuhusu Innocent Kabelwa… halafu Gina, huyu Innocent hili jina siyo geni kabisa," Amata akasema huku akilazimisha ubongo wake urudishe kumbukumbu haraka, "Ikibidi nitapita duka hilohilo ili niwaone kwa uzuri hao watu," akasema.

"Usihofu, kama unahisi unamjua basi utajuana naye tu… sasa tunafanyaje?" Gina akauliza.

"Tutaitembelea hiyo nyumba usiku… maana kutoka hapo tutajua nini cha kufanya," Amata akasema kisha akaendelea kula.

❦


Baa maarufu ya Hangaza ilifurika watu usiku wa siku hiyo. Amata na Gina walikuwa ni kati ya wateja waliojazana humo ndani. Kwa jicho la haraka haraka aliweza kuwaona watu wa kila aina; mafukara kwa matajiri, makahaba kwa wakware. Hangaza ilichangamka haswa utadhani baa mpya. Gina aliinua mkono wake na kuitazama saa aliyokuwa ameivaa. Ilimwambia ni saa saba usiku. Muziki bado ulikuwa ukirindima na waliokuwa kwenye 'dance floor' waliyarudi pasi shaka. Kwa Gina na Amata ilikuwa burudani kuwaangalia watu wakicheza. Wengine walikuwa wamelewa na wengine wazima. Basi kila watu walikuwa na mtindo wao wa kufurahisha. Ilikuwa usiku sana lakini wala hakuna aliyejali. Mauzo ya gulioni yalifanya kazi, mifuko yao ilinukia fedha.

"Oh karibuni sana Ngara," sauti ya mtu aliyejikaribisha mwenyewe pale mezani pao iliyapenya masikio ya wote wawili. Amata na Gina wakamtazama kwa pamoja, kisha wakatazamana wao.
"Asante tumekaribia," Amata akawa wa kwanza kujibu.
"Bila shaka ninyi ni wageni hapa, maana sura zenu tu ni ngeni kabisa. Unajua hapa Ngara tupo watu wachache, tunafahamiana kwa sura na sauti. Zaidi ni rafiki zetu kutoka Rwanda, Burundi, Uganda na wakati mwingine, hata wakongomani hujumuika nasi…"

"Kwanini umesema mnajuana kwa sura na sauti?" Gina akadakiza swali.

"Hapa Ngara tuna vipofu watano wao hutujua sisi sote kwa sauti…" akajibu na wote watatu wakaangua kicheko.

***Itaendelea...***





Kitabu MSALITI kipo madukani, jikamatie nakala yako kwa Tsh 15,000 tu.

Tembelea duka la Kona ya Riwaya Kinondoni au piga

**simu namba 0655428085**
**Whatsapp 0766974865**

Jikamatie nakala yako sasa

# HADITHI: Najutia Kuwa na Wewe—10

**MTUNZI: ASHA SIRAJ**
**Whatsapp 0789044345**



**UTANGULIZI**

**Mapenzi sio kitu cha kuwekea maanani sana kwasababu ipo siku yanaweza kukuletea shida huko mbeleni, kuna baadhi ya changamoto nyingi hutokea. Hivyo ukisema kila jambo uliwekee maanani basi mapenzi yako yatabaki kuwa na majuto siku zote. Kutana na binti SHAZMA aliyepitia mateso mengi kwenye mapenzi yake na kujikuta akijutia kwanini amkabizi moyo wake mwanaume asiye na fadhila**

***Ilipoishia…***

**Niligonga sana hadi nikachoka mkono, ila sauti ya Munira ilisika kwa mbali akiwa anadai kuwa anakuja, nilianza kufurahi kabla hata sijamuona dada angu nilikuwa nimemmiss sana. Nimiaka mingi sasa hatujaonana.**

***Endelea...***

Nilihisi kama anachelewa kufungua mlango maana nilitamani nimkumbatie kwa zile furaha nilizokuwa nazo.

Geti lilifunguliwa na kweli alikuwa Munira nilimsogelea na kumuwao.

“Khaa! kwani we vipi kunukishana kikwapa sahivi?” Munira aliniambia, hadi pozi likaniishia. Niligeuka na kumtazama Shahdu aliyebaki kashikilia mdomo kutokana na yale naneno ya Munira.

“Munira ni’kwamba siku zote hizo ulikuwa hujanimis hadi unafikia kuongea maneno kama hayo?” nikamuuliza.

“Mimi sio Munira yule wa zamani hivyo naomba unitolee shobo zako hapa! Kwanza kimekuleta nini hapa? Hivi Shazma huchoki tu kutufutilia…? Ukweli hatuna ndugu kama wewe, mtu mwenyewe maskini wakutupa.” alilalama.

Daah! Maneno ya dada angu Munira yalizidi kuichanganya akili yangu, hadi niliishiwa pozi. Machozi yalianza kunitiririka nikajikuta nashuka chini taratibu.

Dokta alikuja na kuninyanyua pale, huku akijaribu kuniomba ikiwezekana tuondoke kabla mambo hayajawa mengi. Nilimkatalia dokta nakudai nahitaji kuongea na shangazi wenda yeye akaelewa maumivu yangu.

“Unajisumbua tu hata hivyo mama hana mda nawewe hivyo naomba uondoke mapema, maana nahisi akija hapa anaweza kutapika baada ya kuiona sura yako ilivyo mbaya mpaka inatia kinyaa”. Munira aliongeza kusema.

Nilizidi kulia, “Inaamaana hata wewe Munira bado hujabadilika? Nilidhani hiyo miaka yote utakuwa umebadilika na umetambua uwepo wangu ni muhimu kwenye maisha yenu kumbe ni yaleyale tu!” nikamwambia.

“Nibadilike mimi nimekuwa kinyonga au? Ukweli sisi hatuwezi kukaa na mtu maskini kama wewe Ni sawa unatuingizia mkosi tu ndani kwetu”.

“Munira ila jua hii ni dunia ndugu yangu hapo ulipo huna baba ila hujifunzi hata hilo pia?” nilimuuliza.

“Kipi cha kujifunza hapa kama nibaba tayari ameshakufa haya nini unataka nijifunze labda, em’ nitokee hapa, kwanza mama hayupo hivyo wahi uondoke hapa maana mda sio mrefu atakuwa hapa. Hivyo changamsha kwato zako na utoke hapa,” aliambia.

“Munira siwezi kuondoka hapa bila kumuona shangazi yangu,” nikamwambia tena nilidhidi kufosi, ila sikuwa na uhakika wa kupokelewa na shangazi vizuri.

“Hapa utaondoka!”

“Siondoki Munira!”

Basi mabishano ya mimi na Munira yalianza pale mpaka kupelekea mimi na Munira kuanza kupigana, maana niliona huyo binti hata kama ni dada yangu atanipanda kichwani.

Nilianza kumchezea kipigo pale ukiweka nazile hasira nilizokuwa nazo nilitamani kumvunja mbavu zake na vile alivyokuwa hana mwili ndo’ kabisa sikupata hata pakupiga.

Dokta Shahdu aliingilia kati ugomvi hivyo akaniomba niache. Tulipokuwa tukitaka kuondoka pale, ghafla shangazi aliwasili na kukuta hali sio shwari.

Nilikuwa nishambamiza binti yake hadi uso ushaanza kumvimba, na ukubwa wote aliokuwa nao nguvu za kupigana hakuwa nazo alichojariwa yeye ni mdomo tu.

Kwenye swala la kuongea nikama

alisomea matusi ya kumwaga kama nguo za mitumba. Matusi yalimjaa mdomoni mwake.

"Mwanahizaya wewe umefuata nini nyumbani kwangu?" Sauti ya shangazi ilisikika.
"Shangazi hata wewe pia bado hunithamini kama binti yako?" nikamuuliza.
"Umemfanya nini binti yangu?" akauliza kwa ukali.
"Nimfanye nini shangazi nimempiga kwa sababu hukumfundisha maadili mazuri hivyo imenibidi nikusaidie kumfunza kabla hajafunzwa na ulimwengu," nikamjibu.
Shagazi alinisogelea huku akiunyoosha mkono wake akitaka kunipiga kibao, ila alizuluiliwa na Shahdu. Pale shangazi alibaki kumtazama "wewe ni nani hadi uuzuie mkono Wangu?" Swali la shangazi liliniacha mdomo wazi
"Nilitamani sana kujitambulisha kwenu ila kwa hivi mambo yalikuwa hata nikisema itakuwa vigumu kuweza kunielewa" Shahdu alijibu kwa upole.
"Nivigumu wapi? Hata hivyo naelewa sitaki kusikia chochote kutoka kwako, nyie wote ni malaya tu hamna chakujitambulisha wala nini," aliongea shangazi. Nilijikia vibaya.
"Shangazi sasa naona kabisa unavuka mipaka yako. Tena nakuheshimu ila ulipofikia utanifanya niongee mazito
Mwishowe uweze kunielewa vibaya". Dokta alinishika mkono akiomba tuondoke pale maana mambo yalikuwa mabaya, nahisi hata ngumi pale zingepigwa.


Kiukweli nilijisikia vibaya tofauti na mwanzo mambo yalivyokuwa hata hivyo ni kosa langu ningelimsikiliza Shahdu basi haya yote yasingetokea.
Dokta aliniingiza kwenye gari na kuomba tuondoke pale. Aliwasha gari na kuondoka sauti ya shangazi ilisikika "Ulizani kuna mali zako hapa baada ya kifo cha mume wangu!" ile kauli iliniuma sana.

Yani shangazi kwa roho mbaya aliyokuwa nayo alimzidi hata mama wa kambo. Kiukweli nilijikia vibaya sana safari ilianza, ambayo hata sikuelewa tunaenda wapi.
Niliona aibu kumtazama Shahdu kwasababu ametukanwa kwa sababu yangu, ubishi wangu ndio umesababisha hadi dokta kukasirika.
Nilitamani kumuongelesha ila alionekana kupaniki sana kwa maneno ya shangazi na vile alivyomuita malaya maneno yale yalimkera hata uendeshaji wake wa gari ulikuwa tofauti kabisa na wa mwanzo.

Nilikaa kimya, nilitamani kulia ila nilihisi uwenda nikilia basi nitazidi kumfanya akasirike zaidi.
Sikujua mwisho wa safari yetu ilikuwa ni wapi, ila baada ya kuona bango barabarani likiwa limeandikiwa kimara ndipo nilitambua kwa sasa tupo kimara Temboni.
Baada ya dakika kama tano tuliwasili kwenye mtaa huo wa Kimara Mabibo ndani ya jengo moja zuri la kuvutia. Dokta alishuka baada ya kuwasili getini
Alitoa ufunguo kwenye mfuko wake wa suruali, akaelekea hadi getini kwa ajili ya kufungua. Alifungua lango hilo hadi mwisho lakini mda wote alikuwa kimya.
Alingia ndani ya gari na kuendesha mpaka sehemu alipokuwa anapaki. Alinifungulia mlango wa gari akaniomba nishuke. Sikuwa na neno, nilishuka huku nikishangaa kwa jengo hilo jinsi lilivyokuwa zuri na la kuvutia.

"Utashangaa au utakuja kuchukua vitu vyako?" aliniuliza. Niliamini kweli dokta amekasirika hadi kuongea hivyo. Nini nifanye ili arudi kwenye hali yake. Niliumiza sana kichwa changu nikitafakari namna ya kumfanya dokta atabsamu kama mwanzo. Basi nilibeba mabegi yangu pale na yeye akawa amenisaidia baadhi vitu vilivyokuwa vimebaki kwenye gari.
Aliniomba nimfuate kwa nyuma. Baada ya kuzama ndani ndo nilizidi kushangaa zaidi na kusahau kama ameniambia nimfuate kwa nyuma. Niliposhtuka sikuweza kumuona dokta mbele yangu.
Nyumba ilikuwa na vyumba vingi kona za kutosha hivyo sikujua chumba gani atakuwa ameelekea nilianganza macho yangu huku na kule ilibidi nitulie tu pale.

***ITAENDELEA....***



**SEHEMU YA 1**

## HINDUBAD MBEBA MIZIGO

KATIKA utawala wa Khalifa Haroun Rashid, aliishi katika jiji la Bagdad maskini aitwaye Hindbad. Siku moja, wakati hali ya hewa ilikuwa ya joto kali, Hindbad alipata tenda ya kubeba mzigo mzito kuupeleka mbali sana kutoka sehemu hiyo ya mji ambako aliishi. Alitaabika na joto na uchovu sana, na akiwa bado na safari ndefu ya kwenda, aliingia katika mtaa mmoja ambapo hewa yenye ubaridi mzuri ilipiga juu ya uso wake, na sehemu za kando ya barabara za mtaa huo zilikuwa zikinyunyiziwa na marashi ya waridi. Alifurahi kupata mahali pa kupumzika kama pale, akaweka mzigo wake, na akaketi kando yake, karibu na nyumba kubwa. Madirisha ya nyumba hiyo yalikuwa wazi, na Hindbad aliburudishwa na harufu ya manukato ya kitajiri ambayo yalitoka ndani. vilevile alisikia sauti nzuri ya vyombo vya muziki vya aina zote, vikichanganywa na kutoa sauti nzuri zaidi, na nyimbo nzuuri zilizokuwa zikiimbwa na ndege wadogo wadogo waliokuwa maeneo hayo.

Hindbad hakuwahi kuwa katika sehemu kama ile kabla, na alihisi hamu kubwa ya kujua ni nani mwenyejumba kubwa kama lile na utajiri wote huo na anaeshi kwenye mandhari nzuri sana. alipomuona mtumishi amesimama kwenye lango katika lile jumba zuri, taratibu alijivuta kuelekea kwa huyo mtumishi. Na kwa upole na unyenyekevu, Hindubad akamsalimia yule mtumishi na kuuliza jina la tajiri mwenye jumba hili.

“Inawezekana?” mtumishi aliuliza. “Kwamba wewe ni mgeni sana kiasi ambacho humjui mwenye Jumba hili? Sindubad baharia msafiri maarufu aliyezunguka ulimwengu mzima! Hakuna yeyote katika mji huu asiyemfahamu!” Masikini Hindubad ambaye siku zote alikuwa akisikia utajiri wa ajabu wa Sindubad baharia, kwa huzuni kubwa kabisa aligeuka nyuma na kurudi kwenye ule mzigo wake mzito, akaugemea na kuanza kulia.

“Kuna tofauti gani kati ya huyu mtu mwenye bahati na mimi?” Aliendelea kulalamika mwenyewe. “Kila siku naishi maisha ya tabu na uchovu, mwili wangu umechoka na ngozi inazeeka kwa umasikini uliokithiri, kazi zote ngumu ninazofanya mwishowe naambulia tu mkate kwaajili ya familia yangu, wakati Sindubad yeye anakula utajiri wake na anaendesha maisha yake kwa raha na urahisi kabisa. Ooh!! Jamani, amefanya nini mpaka ametajirika hivi na mimi nina kosa gani mpaka napata shida hii!!”

Alipomaliza kujisemea hivyo, alijiangusha chini kama mtoto anayetaka kitu fulani, huku akilia na kufuta machozi kwa uchungu wa hali yake ngumu sana ya maisha.

Wakati Hindubad anaendelea kuyaendekeza malalamiko yake na huku akinung’unika, akaja mtumishi mmoja kutoka kwenye lile jumba na kumshika mkono na kumwambia kwamba tajiri Sindubad haraka sana angependa kuzungumza naye.

Hundubad alishtuka sana kusikia hivyo, akajua tu kwamba huenda Sindubad amesikia jinsi alivyokuwa akinung’unika na huenda anamuita ili akamsute au akamuadhibu. Basi akajaribu kukataa kwa kutoa kisingizio kwamba ana haraka sana na hivyo asingeweza kupata muda wa kuzungumza, pia alisingizia kwamba hawezi kuacha mzigo wa watu pale barabarani kwani huenda ungeibiwa. Hata hivyo, mtumishi wa Sindubad hakutaka kabisa kusikiliza visingizio hivyo kwani ilikuwa tayari ni amri ya bosi wake, na amri ya bosi wake huwa hairudi nyuma hata kidogo. Kwa kuondoa udhuru huo mtumishi yule aliwaita baadhi ya watumishi wenzake wakae pale nje kwa kuulinda mzigo ule ili Hindubad asipate kisingizio kingine cha kushindwa kuingia ndani kwenda kuonana na Sindibad.

Kisha akampeleka mpaka ndani kwenye holi moja kubwa ambapo kulikuwa na meza kubwa iliyozungukwa na watu waliokaa kama kwenye mkutano fulani hivi. Kwenye meza ile kulikuwa na vyakula vya aina mbalimbali vilivyotengwa kwenye vyombo vya rangi ya dhahabu na fedha.

Mwisho kabisa wa meza ile alikaa bwana mmoja mwenye uso wa heshima mwenye ndevu ndefu nyeupe aitwaye Sindubad!

Uwoga wa Hindubad ukazidi baada ya kuona watu wengi waliokaa katika meza ile, akaanza kutetemeka na kusitasita kwenda. ***Itaendelea...***

**Je unafurahishwa na jarida letu?**

**Tuambie kupitia Whatsapp**

**+255 766 974 865**

# MAONESHO YA 32 YA VITABU TANZANIA
## Vitabu ni Hifadhi ya Maarifa na Utamaduni

Maonesho ya 32 ya vitabu Tanzania yaliyoandaliwa na Umoja wa wachapisha vitabu Tanzania PATA yalifikia kilele chake Jumatano ya tarehe 26 mwezi wa Novemba.

Maonesho hayo yaliyofanyika katika viwanja vya Maktaba kuu ya Taifa Jijini Dar es salaam yalibeba kauli mbiu isemayo 'Vitabu ni Hifadhi ya Maarifa na Utamaduni'.

Maonesho haya makubwa kabisa Tanzania yaliyodumu kwa juma moja yalikusanya wachapisha vitabu, waandishi na wasomaji kwa ujumla ukiachilia mbali wadau wa nyanja mbalimbali ambazo kwazo uhusiano mkubwa na suala zima la vitabu umejengeka.

Katika hotuba yake kwa mgeni rasmi, Mwenyekiti wa PATA Ndugu Hermes Damian aliiomba serikali kutengeneza sera ya vitabu na usomaji nchini. Pia alifikisha ombi kwa Wizara ya Elimu kutoa ufadhili wa kudumu kwa maonesho hayo.

Maonesho hayo yaliyopendezeshwa na mabanda mbalimbali ya wachapishaji, waandishi na asasi za kiraia zinazofanya kazi kwenye uga wa vitabu na usomaji yalikuwa kama baragumu la kuhamasisha usomaji wa vitabu hapa nchini. Makundi mbalimbali ya wapenzi wa vitabu yalifika kujionea na kununua vitabu mbalimbali kwa maarifa na burudani.

Wanafunzi shule za msingi na sekondari hawakuwa mbali katika kuhudhuria maonesho hayo sambamba na wazazi waliofuatana na watoto wao.

Maonesho hayo yaliyofunguliwa na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mh. Prof. Palamagamba Kabudi, yalihitimishwa siku ya Jumatano na Mkurugenzi wa Huduma za Maktaba Dkt. Mboni Uzegeya. Katika hafla ya kufunga maonesho hayo, zawadi za ngao na vyeti zilitolewa kwa mabanda na asasi zilizofanya vizuri.

“Kama zawadi zingalikuwa nyingi basi kila mmoja angekuwa mshindi kwa ushiriki wake” hayo aliyasema Dkt. Nicholous Asheri, mhadhiri wa Chuo Kikuu Dar es salaam aliyekuwa kiongozi wa Kamati ya Utathmini wa maonesho hayo.

Miongoni mwa waliopata zawaddi hizo ni pamoja na Mkuki na Nyota kama mshindi wa wote. Wengine ni UWAVITA katika kipengele cha Inclusivity, Uongozi Institute katika kipengele cha Best Research and Content Exhibitor wakati Room to Read wakijinyakuliwa ushindi kwenye kipengele cha Most Appearing Store for Children.

Ijapokuwa Taasisi ya Elimu Tanzania haikushindanishwa lakini ilipatiwa pongezi nyingi katika kipengele cha mwisho cha Ushirikishi wa Matini kwa kuwa walizingatia hata wale wenye ulemevu.

***Na. Mwandishi wetu...***




**Mwenyekiti wa PATA, Mr. Hermes Damian (kulia mwenye mic) akimuelewesha jambo Mgeni rasmi Mh. Prof Palamagamba Kabudi kabla hajaanza kutembelea mabanda.**

# MAAJABU YA KUSOMA VITABU

Haya ni maajabu machache yaliyofanywa na watu baada ya kusoma vitabu.

**1. Mtu asiyejua kusoma aliyekua mwandishi mashuhuri – Frederick Douglass**

Frederick Douglass, mtumwa wa Marekani, hakuruhusiwa kusoma. Lakini alijifunza kwa siri kupitia kurasa zilizotupwa. Kusoma kulimpa nguvu za akili na ujasiri, na baadaye akawa mwandishi mahiri na mpigania haki za binadamu, hata kuzungumza na marais. Maajabu: Kusoma kulimtoa utumwani kiakili, na baadaye kimwili.

**2. Kitabu kilichobadilisha sayansi yote – "Principia" ya Newton**

Isaac Newton alisoma vitabu vya wanafalsafa wa kale kama Galileo na Descartes. Kutokana na somo hilo, aliandika Principia, kitabu kilichoweka misingi ya sayansi ya leo. Maajabu: Kusoma kulimwongoza kubuni hesabu mpya (calculus) na sheria za mwendo—zilizobadilisha dunia milele.

**3. Msichana aliyesoma sana akaongoza mapinduzi – Malala Yousafzai**

Ingawa alikuwa binti mdogo kutoka Pakistan, kusoma vitabu vilimfungua macho hadi akapata ujasiri wa kuipinga siasa iliyo kataza wasichana kwenda shule. Aliponea shambulio, lakini hakukata tamaa. Maajabu: Leo ni mshindi wa Tuzo ya Amani ya Nobel—hasira yake ilianza kwa kusoma vitabu.

4. **Mwanafunzi masikini aliyekuja kutengeneza kampuni kubwa – Jack Ma**

Jack Ma alipokuwa kijana, alisoma vitabu vya Kiingereza na hadithi za kimataifa, hata bila mwalimu. Hilo ndilo lililomfungulia ulimwengu hadi akaanzisha kampuni ya Alibaba. Maajabu: Kusoma kulimpa maarifa aliyotumia kuwa bilionea bila hata elimu ya chuo kikuu.

**5. Nchi iliyojenga uchumi kwa msingi wa kusoma – Finland**

Miaka ya 1970, Finland ilikuwa maskini sana. Serikali iliamua kuwekeza kwenye utamaduni wa kusoma kuanzia chekechea. Hatua hiyo pekee ndiyo iliyoifanya kuwa miongoni mwa mataifa yenye uchumi imara na ubunifu mkubwa. Maajabu: Taifa likabadilika kupitia nguvu za kitabu

**6. Watoto wa vijijini waliojenga roketi – "The Rocket Boys"**

Kundi la wavulana kutoka mji mdogo wa mgodi Marekani walivutiwa na roketi baada ya kusoma vitabu vya sayansi. Bila walimu wa kitaalamu, walijifunza kupitia vitabu na baadaye mmoja wao akawa mhandisi wa NASA. Maajabu: Ndoto za kwenda angani zilianzia kwenye kurasa za vitabu.

**7. Watu waliobadilisha tabia na maisha kwa kusoma vitabu vya maendeleo binafsi**

Vitabu kama The Secret Letters, Who Will Cry When You Die?, Atomic Habits, Think and Grow Rich vimebadilisha maelfu ya watu—mtazamo, tabia, nidhamu, na mafanikio. Maajabu: Kusoma kunaweza kubadilisha tabia ya mtu taratibu hadi maisha yake yote yabadilike.



# KITABU NILICHOSOMA

## MY LIFE, MY PURPOSE

UCHAMBUZI WA KITABU CHA RAIS MSTAAFU BENJAMIN MKAPA

**"MY LIFE, MY PURPOSE"**

Na PROF. RWEKAZA MUKANDALA

**{Kwa msaada wa mtandao}**

Mtoto Benjamin William Mkapa, alifundishwa kupika chakula na mama mzazi Stephania akiwa mdogo. Alipokwenda shule hapo kijijini Lupaso, Ndanda na hatimaye St. Francis Pugu na Makerere, alifundishwa kupika, kufinyanga, kubuni na kuchambua mawazo na kuyaweka sawa kama msomi mbunifu na mwandishi. Kitabu hiki ni zao la mpishi wa mawazo mahiri aliyebobea. Ni kitabu cha kurasa mia tatu na kumi na tisa, katika sura ya kumi na sita. Kuna utangulizi ulioandikwa na Mheshimiwa Joaquim Chissano, Rais mstaafu wa Msumbiji, Pia kuna picha nyinge nzuri, na viambatisho viwili. Mchapaji Mkuki na Nyota wamefanya kazi nzuri sana, sikubaini kosa hata moja.

Wasilisho hili linamega simulizi hii katika sehemu kuu tatu. Kwanza tunapewa vionjo vitamu tukielezwa kuzaliwa kwake, kukua na kwenda shule. Hii ilikuwa matayarisho ya kufikia nia au azma yake ya maisha. Kisha tunaletewa mlo wenyewe (main course) uliosheheni kumbukumbu na ngano za huyo kijana sasa mtu mzima akiwa kazini, mpaka akaukwaa urais wa Tanzania. Mwisho tunaelezwa kwa ufupi maisha yake baada ya kumaliza ngwe yake ya miaka kumi ya urais.

**2. KUZALIWA, MALEZI NA ELIMU**

Baba yake mzazi Mheshimiwa Mzee William Matwani alikuwa mpishi msaidizi huko Mission Ndanda. Wamisionari wakambatiza, wakamfundisha kusoma, kuandika na kuhesabu, na kumfanya Katekista. Alipelekwa Lupaso, ambapo alieneza dini na kufundisha Bush school ya Wamisionari. Alimwoa Bibi Stephania Nambanga ambaye hakujua kusoma wala kuandika. Walijaliwa watoto wanne Benjamin akiwa wa mwisho. Kama ilivyo kwa kabila la Makua, Benjamin alipewa jina la ujombani, Mkapa. Mama hakuwa na muda wa kujifunza kusoma na kuandika kwani yeye ndiye alikuwa msingi wa familia, akihakikisha analima, kulisha familia, na kuwalea watoto. Alikuwa mkali lakini msikivu na mpenda haki. Wazazi hawa ndio vinara wa sehemu hii ya kwanza ya simulizi hii. Waliishi pamoja kwa uadilifu na heshima kubwa, na mapenzi ya pamoja kwa watoto wao.

Ingawa wazazi hawakwenda shule, walipenda sana watoto wao wote waende shule. Hii pamoja na kwamba Baba Matwani alikuwa na kipato kidogo lakini cha uhakika kila mwezi, kiliifanya familia ionekane iko tofauti. Hii ilipelekea wivu na hatimaye chuki kutoka kwa jamii. Wivu huu na chuki ulisababisha tukio moja baya sana ambalo Mheshimiwa Mkapa analikumbuka kwa uchungu. Mwaka 1947, kulitokea ukame mkali, basi watu wakamleta mganga wa kienyeji akaamua kuwa mama mzazi, mama yake na bibi yake ndio walikuwa wameloga na kuzuia mvua. Walipigwa na kuteswa sana hadi Padri Mzungu alipofanikiwa kuwanasua. Bibi wa mama aliaga dunia muda mfupi baada ya tukio hilo.

Kijana Benjamini na mwenzie mmoja ndiyo waliopata bahati ya kuendelea na masomo ya Sekondari, kutoka darasa la watoto 25 hadi 30. Kuchaguliwa ilikuwa bahati nasibu.

Shule ya sekondari ya Ndanda ilikuwa kilometa 60 kutoka Lupaso. Yeye na wenzie walitembea kwa miguu, bila viatu, kwa siku mbili, wakiwa wamebeba kichwani vitu vyao ambavyo vilikuwa vimefungwa katika mkeka. Baadae alipata sanduku la chuma.

Walimu wa Ndanda walikuwa wamisionari na walikazia sana sala na kazi “Ora et labora”. Wanafunzi walipika chakula chao wenyewe. Kwa kuwa kijana Benjamini alikuwa mdogo sana alipewa kazi ya kuosha vyombo. Kawaida alivibeba vyombo kichwani mpaka mahali pa kuvioshea, na kuvirudisha. Anasema kubeba vyombo hivyo ndiyo sababu ana upara hadi leo

Mwaka 1952, akiwa na umri wa miaka 15, aliamua kwenda Seminari darasa la nane. Baada ya muda mfupi aliamua kuwa upadre haukuwa wito wake, akarudi Ndanda kuendelea na shule. Mwaka 1957, alichaguliwa kwenda St. Francis College Pugu ikiwa ni shule kuu ya Wakatoliki Tanganyika. Akiwa Pugu, kijana Benjamini alianza kupata mwamko wa kisiasa. Aliunga mkono harakati za kupata uhuru kwa kuandika barua kwa Mhariri wa Gazeti la “Tanganyika Standard” ambalo sasa ni Daily News akiunga mkono hoja ya Uhuru. Barua ilichapishwa. Ila kijana Benjamini alitumia jina bandia!

*Itaendelea...*

# HABARI PICHA



Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo Mh. Prof Palamabamga Kabudi akifungua Maonesho ya 32




Mh. Prof. Palamagamba Kabudi akisikiliza neno kutoka kwa Mwenyekiti wa PATA

Moja ya zawadi iliyovuta hisia za watu iliyotolewa na Mwl. Richard Mabala kwa Mwenyekiti wa PATA .






Wazungu nao walikuwepo kujionea uandishi wa Ki-Tanzania



Katika banda la Mkuki na Nyota... Tabasamu ilitawala

Waandishi bunifu katika picha ya pamoja na mgeni rasmi siku ya kufunga kwa Maonesho ya 32 ya Vitabu




**TANGAZA na NGURUMO YA MWANDISHI kwa bei nafuu na ya kirafiki.**
**Matangazo madogo ni Tsh 5000@ na Tangazo la kurasa nzima ni Tsh 10000@.**
**Wasiliana nasi kwa simu *(call & Whatsapp)* 0766974865 na Email: jamvilasimulizi@gmail.com**

## TANZANIA MAMA YETU

Tanzania mama yetu, kwa moyo twajivunia
Amani ni tunu yetu, jirani waikimbilia
Shida nini mwanakwetu, hata twaipuuzia
Tanzania mama yetu, maziwa twafaidia.

Tazama kushoto kulia, nani nawe alia
Tabaki peke twalia, ujinga mejitwalia
Hii ni yetu Tanzania, twapaswa kujivunia
tanzania mama yetu, maziwa twafaidia

Uchu umewajaa, majirani zungukia
Ni kama wana njaa, mabaya watutakia
Waona nyota ya jaa, kuipata Tanzania
Tanzania mama yetu, maziwa twafaidia.

Mungu ametujalia, mali nyingi asilia
Lakini tunacholia, wachache kujifaidia
Ni yetu wote Tanzania, na si chache familia
Tanzanaia mama yetu, maziwa twajifaidia.

Wajanja wautumia, uchungu ulotuamia
Amani tuvurugia, na kubaki twaumia
Jitafakari Tanzania, nani tutamlilia
Tanzania mama yetu, maziwa twajifaidia.

Tutunze nguvu vijana, tuijenge Tanzania
Nguvu si za kupigana, nchi kujivurugia
Bali tukishikamana, mengi tutajivunia
Tanzania nchi yetu, maziwa twajifaidia.

Shimeshime Mtanzania,  akili yako tumia
Tawi ulilokalia, utakuja jivunjia
Nani utamlilia, chini ukiangukia
Tanzania nchi yetu, maziwa twajifaidia.

**Shujaa Maneno**
**Bagamoyo—Pwani**

## HUYU NI WANGU AYUNI

Huyu ni wangu ayuni
Kamwe aso majinuni
Baya lake kwangu ubani
Kama tunda ye zaituni

Mtamu wa utamuni
Uchungu kwake uhaini
Pambaja ziso kifani
Kajaza jazia uani

Maneno matamu kinywani
Matiti konzi kifuani
Utunda mwingi kiunoni
Utamu bwere pajani

Akilala namtamani
Akiketi ni unyamani
Akiinama shambani
Nasimama maungoni

Alomsawiri nani
Malaika au shetani
Kamjaza mambo ya Pwani
Utosini hadi nyayoni

Hili ni balaa gani
Mbinguni na duniani
Binadamu au alieni
Mtamu nje na ndani

Loh!

**Laabib A. Zuberi**
**Zanzibar—Tanzania**

**Unaweza kuchangia chochote ili kuwezesha jarida hili kuwa bora na kuwafikia wengi zaidi. Kama upo tayari, changia kiasi chochote kupitia MPESA LIPA NAMBA 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Na Mungu atakujazi.**


new text
KAMANDA AMATA
OPERESHENI KASHMIR
OPERESHENI KASHMIR
Sasa Kinapatikana kwa Tsh
15,000/=
JIKAMATIE
NAKALA YAKO
DAR ES SALAAM
Duka la Kona ya Riwaya
Kinondoni Morocco
Simu:
0655428085
Zammira


KAMANDA AMATA
MSALITI
"Kamwe hatoki upande wa adui yako"
MSALITI
15,000/=
Kona ya Riwaya
BOOKSHOP
Fika dukani kwetu au wasiliana nasi Kwa Simu
0655 428 085
Mliopo mikoani tunakutumieni.


KINAPATIKANA
ARUSHA
Kinapatikana Kwa Ally Said Shaban, nje tu ya KIMAHAMA Bookshop
Simu: 0757690302 na 0656744390
KAMANDA AMATA
MSALITI
15,000/= tu
Jipatie Nakala Yako Sasa!


new text
KAMANDA AMATA
OPERESHENI KASHMIR
OPERESHENI KASHMIR
Sasa Kinapatikana kwa Tsh
15,000/=
JIKAMATIE
NAKALA YAKO
ARUSHA
Nje ya Duka
KIMAHAMA
Simu
+255 757 690 302
ALLY SAID

# KUTOKA MAKTABA
# MWANDISHI WA ENZI HIZO: 2. AGORO ANDURU

KUTOKA MAKTABA leo tunamzungumzi mwandishi nguli wa fasihi ya Kiingereza na hata Kiswahili. Huyu si mwingine, ni Mtaznania Agoro Anduru.

Hebu basi tumjue…. Agoro Anduru alizaliwa mwaka 1948. Alitoka kijijini kando ya Ziwa Victoria *(shores of Lake Victoria)*, eneo ambalo sasa ni sehemu ya Tanzania. Alipata elimu ya msingi na ya awali katika shule za kienyeji — ingawa alipitia changamoto za usikivu (partial deafness), jambo alilielezea mwenyewe kwenye moja ya hadithi zake.

Changamoto hiyo ya usikivu ilimlete shida alipokuwa shule lakini hakukubali kushindwa; badala yake ilimpa mtazamo maalum juu ya maisha — uzoefu ambao baadaye ulifanya iwe rahisi kwake kuangalia mahali penye huzuni, kutambua udhaifu wa jamii, na kuyabadilisha yote kuwa hadithi.


**Kazi na maisha kama mwandishi**

Kabla ya kuwa mwandishi wa hadithi fupi, Anduru alifanya kazi kama mtangazaji wa redio *(radio journalist)*.

Uandishi wake ulianza kulipuka miaka ya 1970, wakati hadithi zake zilipoanza kuchapishwa katika magazeti ya ndani — mfano, gazeti la hapo zamani likiwa ni moja ya njia za kueneza kazi zake.

Katika kipindi cha miaka ya 1980, aliandika na kuchapisha miswada kadhaa ya hadithi fupi na riwaya za somo la kijamii kwa lugha ya Kiingereza na pia Kiswahili — jambo ambalo lilimweka kama mmoja wa waandishi wa mwanzo wa fasihi ya *"Anglophone"* Tanzania.

Kazi zake ziliangazia maisha ya mijini, matatizo ya kiutu, maadili ya kijamii, migogoro ya hisia — kwa njia ya uandishi wa kisanii.



AGORO ANDURU

**Kitabu / Mkusanyo Lugha / Aina Tarehe / Maelezo**

**This Is Living: And Other Stories** Hadithi fupi (English) 1982

**A Bed of Roses and Other Writings** Hadithi / Maandishi (English) 1989

**Temptation and Other Stories** Hadithi fupi (English) 1981 (mid-1980s)

**The Fugitive** Hadithi / riwaya fupi (English) ilitajwa miongoni ya kazi zake maarufu

**Kukosa radhi (Without Blessing)** Novella / riwaya ya Kiswahili 1983 — mfano wa kazi yake kwa Kiswahili na sehemu ya fasihi ya maarufu ya *"pulp/ popular fiction"* ya Tanzania.

**Changamoto & Ukosefu wa Hifadhi**

Licha ya mchango wake, kazi za Anduru hazikuwekwa vizuri katika mifumo ya uchapishaji au maktaba — hivyo leo ni vigumu sana kupata vitabu vyake mara moja. Kazi zake nyingi zimekuwa *"out of print"* au zimepotea kabisa.

Fasihi ya waandishi wa lugha ya Kiingereza nchini Tanzania (ya enzi hizo) haikutambuliwa sana kama "mtazamo mkuu" — hivyo kazi kama yake mara nyingi haikuhifadhiwa kama ilivyokuwa kwa waandishi wa Kiswahili.

Ingawa alijaribu kuandika pia kwa Kiswahili *(kama inavyoonekana kwenye Kukosa Radhi)*, hisia ya "fasihi ya kitaalamu" pia ilifuata lugha ya Kiingereza — kwa hivyo kazi zake mara nyingi haikupata hadhira kubwa kama ilivyostahili.

**Mchango na umuhimu wake**

Agoro Anduru anahesabiwa kuwa mmoja wa waandishi wa mwanzo wa fasihi ya Kiingereza *(Anglophone)* nchini Tanzania — na hivyo sehemu ya historia ya fasihi ya Tanzania inamtambua.

Kazi zake zilikuwa na mtazamo wa kijamii — kuangazia maisha ya kawaida, tabia, mabadiliko ya miji, na changamoto za kiutu — tofauti na uandishi wa kifasihi kilichoelekezwa tu kwenye sehemu za utamaduni au kisiasa. Hii inafanya kazi zake kuwa na thamani ya kihistoria na kijamii.

*Itaendelea toleo lijalo….*

## SAFARI YA MALEZI 7: MITINDO YA MALEZI

**SAFARI YA MALEZI 6:**

**6.0 Mitindo ya Malezi**

"Watoto ni kama mimea midogo; malezi wanayopokea huamua jinsi watakavyokua." Malezi huunda tabia, utu, na ukuaji wa mtoto kwa ujumla. Katika kazi hii inaonyesha aina tatu za mitindo ya malezi: Malezi ya kisheria/ kijeshi *("autocratic method"),* malezi ya uhuru *("permissive method'),* na malezi ya kidemokrasia *("democratic method").* Ambapo katika kila mtindo tutaangalia maana yake, faida zake, hasara zake, na mifano halisi ya maisha ya kila siku. Lengo ni kuangazia jinsi mbinu hizi zinavyoathiri ukuaji wa mtoto, uamuzi wake, na hisia ya uwajibikaji. Inaonyesha njia mbalimbali ambazo wazazi wanavyowaongoza, kuwatunza, na kuwaadhibu watoto wao, ikionyesha matokeo ya kila mbinu katika maisha halisi.

**6.1 Mitindo au Aina za Malezi**

**6.1.1 Malezi ya Kijeshi *(Autocratic Parenting)***

Na. KELVIN JOHN KYARA

0753767930

Haya ni yale malezi ambayo mzazi anatoa amri kwa mtoto na kutaka ifuatwe bila kuulizwa. Mzazi huweka sheria, masharti, na vikwazo vilivyowekwa wazi, na mara nyingi hutumia zawadi au adhabu kuhakikisha watoto wanafuata. Kila jambo linapangwa na mzazi: watoto wafanye nini, wapi wafanye, lini wafanye, na jinsi ya kufanya. Hakuna nafasi kubwa ya kuuliza maswali au kushiriki maamuzi, na mara nyingine mtoto hajui ni lini anaweza kufanya kitu kwa hiari yake.

Katika aina hii ya malezi zipo faida chache ambazo ni; kumjengea mtoto nidhamu, mtoto kujifunza kufuata maagizo na sheria bila kuchelewa. Kwa mfano, mtoto anayesafisha chumba chake kila siku kama ilivyopangwa na mzazi anajifunza mpangilio na nidhamu ya kila siku. Pili kuelewa mipaka, kwa kuwa sheria na masharti yametolewa wazi, mtoto anajua kipi kinachoruhusiwa na kipi kinachokatazwa, jambo linalomsaidia kuelewa jinsi jamii inavyofanya kazi. Tatu, kumuhakikishia mtoto usalama, Mzazi anayesimamia kila hatua ya mtoto anaepuka hatari ambazo zinaweza kutokea kwa kutofahamu au kufanya mambo hatarishi.

Pia zipo hasara za mtindo huu wa malezi ambazo ni, hofu na ukosefu wa kujiamini, watoto wanaweza kuogopa wazazi au kushindwa kufanya maamuzi yao wenyewe, wakihofia kuharibika au kupata adhabu. Pili Kupungua kwa ubunifu, kwa kuwa kila kitu kinasimamiwa, mtoto hawezi kutumia mawazo yake au kujaribu njia mpya za kutatua tatizo. Tatu, mawasiliano dhaifu, mazungumzo kati ya mzazi na mtoto yanaweza kupungua, kwa sababu maoni ya mtoto hayathaminiwi.

**6.1.2 Malezi ya Uhuru *(Permissive Parenting)***

Hii ni aina ya malezi ambapo mzazi anaruhusu mtoto kufanya mambo kwa uhuru wake mkubwa. Sheria na vikwazo ni vichache sana, na mara nyingi hakuna masharti makali yanayolazimisha utii. Mtoto anapewa nafasi ya kuchagua, kujaribu, na kujifunza kutokana na matokeo ya vitendo vyake mwenyewe. Mtindo huu unalenga kumpa mtoto uhuru na kujitegemea katika maamuzi madogo ya kila siku.

Tuangalie faida za mtindo huu wa malezi: Moja, kuendeleza fikra za kibunifu, mtoto hufikiria njia tofauti za kufanya jambo, akijifunza mbinu mpya. Mfano: mtoto anapewa ruhusa ya kuunda mradi wa sanaa wa shule kwa mbinu yake mwenyewe, akitumia rangi na vifaa vyovyote



UHURU unapozidi kwa watoto. (picha kutoka mtandaoni)

anavyopenda bila kusimamiwa. Pili, kuimarisha uhuru wa maamuzi, mtoto anajifunza kuchagua na kubeba matokeo ya maamuzi yake. Nyingine ni, mawasiliano mazuri kati ya mzazi na mtoto, kuongeza kujitegemea.

Hasara za aina hii ya malezi, ni ukosefu wa nidhamu na mpangilio, kwa kuwa vikwazo vipo vichache, mtoto anaweza kutojua mipaka au kushindwa kuishi kwa mpangilio. Pili, kuzidi mipaka na hatari. Uhuru mkubwa unaweza kumfanya mtoto kujaribu mambo hatarishi. Mfano: mtoto anaweza kuenda kucheza kwenye maeneo hatarishi bila uangalizi wa mzazi au kutumia vifaa hatarishi bila mwongozo. Tatu, kutokuwa na ufahamu wa mipaka ya jamii, kwa kuwa mtoto amezoea kufanya mambo kwa uhuru mkubwa, anaweza kushindwa kuelewa mipaka muhimu ya kijamii. Mfano: mtoto haelewi vizuri vigezo vya heshima au kufanya kazi kwa timu, akidhani kila kitu ni kwake binafsi.

### 6.1.3 Malezi ya Kidemokrasia *(Democratic Parenting)*

Hii ni aina ya malezi ambapo mzazi anachanganya mpangilio wa nidhamu na uhuru wa mtoto. Mzazi ndiye kiongozi wa familia, lakini pia anakazia ushirikiano, mazungumzo, na kushirikiana kwa maamuzi madogo ya kila siku. Mtoto anapewa nafasi ya kutoa maoni, kushirikiana katika maamuzi, lakini ndani ya mipaka iliyo wazi. Hii inasaidia mtoto kujifunza uhuru ndani ya nidhamu, ubunifu, na uwajibikaji.

Mojawapo ya faida muhimu ya aina hii ya malezi ni mtoto anapata uhuru wa kuchagua lakini ulio na kikomo na uangalizi, pili kuendeleza uongozi na ushirikiano, mtoto anajifunza kushirikiana na wazazi na ndugu katika kupanga shughuli. Mfano: familia inakaa pamoja kupanga ratiba ya wikendi, kila mtoto anatoa maoni yake, na mzazi anachanganya maamuzi. Tatu, Kuimarisha mawasiliano ya wazi, watoto wanaweza kueleza mawazo na hisia zao bila hofu, wakifahamu wazazi wanasikiliza. Mwisho, Kujifunza uwajibikaji, watoto wanajifunza kuchukua matokeo ya maamuzi yao ndani ya mipaka. Mfano: mtoto anapewa nafasi ya kupanga muda wake wa masomo na michezo, na anajua lazima atimize kila jukumu.

Athari inayoweza kujitokeza katika mtindo huu wa malezi, ni mchanganyiko unaweza kuchanganya baadhi ya Watoto. Baadhi ya watoto wanaweza kuhisi hofu au kuchanganyikiwa kati ya mpangilio na uhuru. Mfano: mtoto anaweza kushindwa kufanya kazi kwa wakati uliowekwa kwa sababu anajaribu kufanya mambo yote kwa uhuru.

**Mwandishi na Watoto Wake**

Basi bwana! Leo nikawapeleka mabinti zangu pale Maktaba Kuu Ya Taifa, kwenye Maonesho ya 32 ya Kimaitaifa ya Vitabu. Mabinti walifurahia sio tu vitabu *(wamekwangua akaunti, si kidogo!)*, bali pia, kukutana na watunzi wakubwa wanawake nchini - nawaongelea mwenyekiti wa Kamati ya Tuzo Taifa ya Mwl. Nyerere ya Uandishi bunifu, Prof. Penina Mlama, Nahida Esmail na Sauda Simba
Ilikuwa poa mno!!



**Hussein Issa Tuwa**



# HAPPY NEW YEAR '12'—Twahir Yusuph

*Ilipoishia...*

**"Vijana wale watatu, wakaanza kumuingilia kimmm..mwili Mona wangu, tena wakimrekodi na kutaka wazazi wake tuone." hapa alilipiga piga shoka laje sakafuni kwa uchungu huku akilia. "Siiii..iiwezi kuuhadithia, au japo kuu..u..elezea tu kwa ufupi, nnn..ni uchungu kiii..aasi gani ambao mioyo yetu mimi na mke wangu uliuhisi.**

*Endelea…*

Masikio yetu yaliisikia kila kelele ya Mona wetu akilia wamwache, hataki, zaidi akipaza yowe kuwa anakufa" hapa akalia kwa maumivu mno. "Nyi..iiie hammm..muwezi kuyajua machozi yale yalivyokuwa mazito, hadi mboni zetu kufunga kwa kushindwa kuendelea kuutazama unyama ule, binti yetu akiwa anabakwa zamu kwa zamu na vijana wale washenzi." aliutupia mkono ambao haukushika shoka usoni, akiifunika sura yake kwa simanzi na hasira. "Ndiyo, Mona wetu alibakwa, tena sio tu hivyo, walimlawiti pia mimi na mama yake tukilazimishwa kushuhudia tukio lile huku wakitutamkia HAPPY NEW YEAR! HAPPY NEW YEAR! HAPPY NEW YEAR! Kila walipokuwa wakitimiza haja zao kwenye mwili wa Mmoo..ona wetu."

"Basi ni bora wangemfanyia vyote kisha wakamuachia uhai wake waliouvua thamani. Kitendo chao kiovu kilipelekea kifo kwa binti yetu mrembo. Binafsi hata usingizi uliogopa kunisogelea usiku huo, sikulala. Siku iliyofuata, nikiwa mbele ya runinga ambayo sikuizima, mbele ya Laptop iliyonionesha sura nzuri ya binti yangu kwa mara ya mwisho, na hadi ufedhuli aliofanyiwa. Mbaya zaidi, ni mbele ya mwili wa mke wangu aliyetorokwa na roho yake kwa presha ya tukio la mwanawe kipenzi, akiwa mapajani mwangu amelala usingizi m'baya kabisa, usingizi wa milele ambao haukumfanya aamke tena hadi leo.." alishika tama, akayamwaga machozi tele kwa uchungu. "Runinga ile ilitangaza taarifa za msichana mmoja kukutwa barabani amelala akiwa haongei, milango ya mboni zake imefunga, hakuna kiungo cha mwili wake ambacho kilitikisika kwa fahamu zake mwenyewe, hata mavazi aliyovaa yote yalikutwa yamelowana damu." Hapa akatabasamu kwa hasira, akijifuta machozi kwa viganja vyake.

"Ilisadikika amegongwa na gari hadi mauti kumkuta, kisha dereva akatokomea kusikojulikana." akacheka kwa huzuni, akiliachia shoka lake lililotoa kishindo baada ya kudondoka na kutua sakafuni. "Eee...eti mwanangu mimi nd..ii..iye aliyegongwa na gari hadi kufa, ni binti yangu niliyemshuhudia akib..baakwa na kulawitiwa hadi malaika akaingilia kati na kuibeba pumzi yake irudi kwa aliyemuumba, ili asiendelee kuteseka na kudhalilika. Kubwa zaidi walim'badili hadi nguo" hapa mboni zake zote zilionesha kutiririsha machozi mfululizo. "Pumzi zilisham...saliti binti yangu, haaa..kuwa na maisha tena. Yeye na mama yake woo..ote waliniiii...acha usiku mmm..moja." akalia sana, akamwaga sana machozi bwana muuaji, huku kigugumizi cha huzuni kikiendelea kumshika. "Mimi Wiii..izard Gaino." hapa aliongea akitetemeka kwa kilio, huku akijipigapiga ngumi kifuani kwa uchungu uliomtawala. "Nilijilaani kwa kuwa baba asiyejali, baba muoga asiyeweza kutoa msaada hata kwa familia yake mwenyewe, pindi binti yangu mpendwa alipolia kwa maumivu, tena akilalamika kwa uchungu akiniita baa..aba yake nimsaidie..." kimya kikamvaa, alishindwa kuendelea, kiti kikawa kibaya tena, aliifuata sakafu na kuikalia huku mboni zake zikiyamwaga machozi mengi bila kujizuia.

"Nilimzika mke wangu, ila binti yangu hata maiti yake sikwenda kuitazama, nilitaka kuipigania haki yake kwanza, kisha ndiyo ningemsitiri pahala pema ambapo alipastaahili. "Niliiamini sheria, kimbilio langu lilibaki mahakamani, mi niliipinga hadharani ajali yao ya gari waliyoinadi kuyaiba maisha yake, ni uu..ongo ule.." aligugumia kwa kilio, machozi yakimtiririka. "Laiti ningefahamu mapema kuwa vijana wale watatu walikuwa watoto wa watu wenye ujabali mno ndani ya Taifa hili la Takaseni, basi ningeitumia njia hii bila kuwasumbua namna ile, nisingefanya yote yale yaliyotiwa upofu sababu ya nguvu za ki'mamlaka walizonazo. *Hey* rafiki zangu watatu, nyinyi wenye viatu vikubwa vinavyoikanyaga sheria mnavyotaka ndani ya nchi hii." aliwaita CDF Rashidi Koboko, IGP Edward Kituo, pamoja na baba wa Labi Kimati. "Mi sijasahau mlivyonipa pesa

nyingi ili niifute kesi mliyoamini ingezitia dosari familia zenu, na nyadhfa mlizonazo mkizithamini. Laa..abda ule kwenu mliutafasiri kama utu mnaoumudu kunifanyia, au pengine ulikuwa upendo wenu mkubwa kwa wanenu, uliowanyima nafasi ya kutambua hata mimi nilikuwa baba pia kwa mwanangu! Mume vilevile kwa mke wangu aliyedhurumiwa maisha yake, baada ya udhalimu walioutenda watoto wenu kwa binti yetu huku tukishuhudia."


"Nilipowakatalia fedha zenu, nyie mlivyo mabeberu mkampandikiza daktari mliyemlipa pesa nyingi ili atoe vipimo vya uongo, hata hakimu wa kesi ile pia aliwasujudia nyinyi. Bahati yake sana yamemuua maradhi, ila mi sijamsamehe mbwa yule." akajifuta machozi, huku akikamata tena shoka lake na kuinuka, sasa alisimama wima. "Mliponishinda mahakamani, sikuwa na cha kufanya zaidi ya kuupumzisha mwili wa mrembo wangu Mona, ulionibubujisha machozi mengi kila nilipoutazama pale monchwari nilipoufuata, ziliponijia picha za tukio lile la kinyama alilotendewa nikiona. Kwa udhaifu nilionao nilishukuru, nikaiacha huzuni ikinipiga vibao vingi vya manyanyaso, ilivyozitesa hisia zangu kwa machozi yaliyoniuma hadi sio vizuri. Kumbe nyinyi hamkutosheka, mkayahitaji na maisha yangu ili nafsi zenu ziishi kwa amani na usalama mpana kwenye ardhi hii. Mungu akawafanikisha vijana wenu kuniteka, wakanitesa sana muda ambao nikiyatumikia mateso mengine ya kuporwa wapendwa wangu. Nikiwa ndani ya kiroba na uhai wangu wa kutetereka, wakanitupa baharini wakiamini wamefikia suluhisho la kila walichokitaka." akacheka kwa hasira, machozi yakimdondoka na kutua kwenye sakafu aliyoikanyaga.

"Sijui Mungu alimficha wapi msamaria mwema yule, dakika chache baadae nilijikuta nje ya maji waliyojipa uhakika kuwa yangeuzamisha uhai wangu. Niliokolewa na mvuvi, na nilipona hivyo, japo niliishi kama mfu baada ya kurudi ulimwenguni." Baada ya kuongea hayo akavuta pumzi ndani mithili ya mtu mwenye pua zilizozongwa na kamasi. Kisha viganja vyake vilivyolishikilia shoka lake vilikaza kwa nguvu, huku mboni zake zenye lenge kubwa la machozi na hasira zikimgeukia Labi Kimati aliyemfunga kitini. "Kwanini mlimbaka mwanangu Labi, *Why* mlimtendea unyama ule mliotuonesha hadharani vile, niambie maana ya kutuimbia nyimbo za HAPPY NEW YEAR kwa fedheha namna ile." kinyonge sana aliuliza akilia, huku akinyanyua shoka lake juu kwa mkono wake wa kuume. "Sema Labi?" alifoka na kulitua shoka lake shingoni mwa Labi Kimati. Kilichofuata kilitisha mno, alifanya kama yupo buchani, kila shoka lililotua mwilini mwa Labi Kimati aliye marehemu saa hiyo, liliongozana na swali la kumtaka aelezee sababu ya anachoulizwa. Unyama na ukatili ulitendeka huku kamera ikiwa wazi na kuendelea kurusha tukio hilo mtandaoni. CDF Rashidi Koboko, IGP Edward Kituo, na baba wa Labi Kimati wote walikuwa mashuhuda. Nyuso zao zilitekwa na huzuni kila mmoja pahali alipokuwepo saa hiyo, haswa paji la mzee Kimati Sesewa.

Machozi yalimchuruzika kwa fujo, kelele, na simanzi kubwa asiyoihimili. Ni ndani ya jumba lake la kifahari bwana Kimati Sesewa akiwa juu ya kochi, viganjani akiikamata simu yake iliyomwonesha tukio hilo la kutisha, alilia mno. Alimlilia kijana wake aliyezidi kuulizwa swali moja tu, huku shoka likiendelea kutua kwenye mwili wake ambao ulishaachana na roho kitambo tu. Kwa Vivi ilikuwa zaidi ya majonzi, pete aliyovishwa hivi karibuni haikuwa na maana tena. Labi wake amepelekwa ulimwengu mwingine. Kama ni ndoa anaweza kuipata lakini sio kwa mwanaume huyo aliyependana naye. Alilia mara nyingi Vivi, kumpoteza Labi, kuikosa Ndoa, na kuijua simulizi mbaya ya nyuma inayomuhusu Labi wake, kumbe alikuwa akienda kuolewa na mwanaume mnyama na mkatili kiasi hicho.

Alilia mno akiwa chumbani kwake juu ya kitanda, nyumbani kwao. Ni zaidi ya unyama, uliofanywa na muuaji huyo ambaye alishalitaja jina lake kuwa ni Wizard Gaino.

*Itaendelea...*



# RIWAYA: NGUVU YA KIAPO (07)- Na: Eva Mrema

*Ilipoishia…*

**Kwa ulimi laini akaniomba anioe. Sikuwa na jibu, machozi yalianza kunibubujika nilitoka karibu yake na kukimbilia msalani. Nilifungulia maji na kuanza kulia kwa kwikwi.**

*Endelea…*

Nilimsikia Sunche akinigongea mlango na kuniita kwa kukazana sana. Nililia tani yangu. Nililia hadi nilipohisi wepesi wa nafsi. Nilitota kwa maji kiasi cha meno kuanza kusagana kwa ukali wa baridi. Niliufungua mlango huku natetemeka. Sunche alinitazama kwa huruma. Alinifunika kwa taulo na kunikumbatia. Alinituliza.
Baada ya muda kupita nilitulia. "Mpenzi, nataka kukusikiliza. Nataka useme yote ya moyoni ili nikuhurumie na nikiweza tukubaliane kuyabatilisha." Sunche aliniambia. "I'll be okay darling! Nilimjibu huku nikijiweka sawa na kuyalalia mapaja yake. Alininyanyua na kunitazama machoni."Nataka tuongee Tabita" alisisitiza.



Nilijifikiria kwa sekunde chache kisha nikapiga moyo konde na kufanya maamuzi ya kufunguka. "Sawa, kama uko tayari kunisikiliza bila kunihukumu nitakueleza yote"
"Sijui nianzie wapi" Nilijitafuna sana Sunche alinitazama, "unaniamini?" Aliniuliza. Nikajibu Ndio bila kuufungua mdomo wangu, nilitingisha kichwa tu. "Ongea na mimi Tabita" Sunche aliongea kinyonge sana. Nilivuta pumzi ndefu na kuishusha. Nikajiambia tu, "kama sintoutua mzigo ulionichosha kwa kitambo, sintokuwa na nafasi ya kubeba mzigo wa kunifaa" "Sawa, nitasimulia kwa sharti moja" niliongea huku namtazama Sunce aliyenipa umakini wake wote. "Naomba uniache hadi nimalize kabisa kusimulia ndipo utie neno" Sunche hakuwa na pingamizi.
"Ni miaka mitatu imepita tangu linikute la kunikuta, nilipoteza marafiki na jamaa zangu wa karibu, nilimuathiri sana mdogo wangu ambaye alikuwa na mimi tu. Hadithi yangu na Pharao ilianza kitambo, nikifanya kazi kwenye ofisi ya mkuu wa wilaya, Babati. Makutano yetu ya bahati mbaya zaidi ya mara moja nilikuja kubaini baadae sana yalikuwa mpango ovu wa Pharao. Alihakikisha ananiteka kwa penzi lake nililoliamini sana. Na mimi kama kipofu nisiyejua uelekeo, nikipenda ninapenda Sunche. Nilimpenda yule jamaa. Tulidumu kwa miezi mitano tukiwa wa moto sana. Alifanya kazi uwanja wa ndege Kisongo, mimi na yeye tulionana kila mwisho wa juma. Tuliapizana viapo vya uaminifu. Tulipeana ahadi lukuki. Wakati huo nilikuwa ninajenga. Mdogoangu alikuwa akiishi shule, likizo alikuja nilipokuwa nimepanga.

Nilimaliza ujenzi na kuhamia nyumbani kwangu. Mambo hayo yote Pharao aliyajua. Na mimi niliijua mipango yake mingi ya maendeleo aliyonijuza kwa hiyari yake. Kiukweli, mbali na mapenzi niliiona kesho yetu yenye mafanikio pamoja. Nilimuhesabu kama mwanaume mpambanaji. Sikusita kusaidia alipoonesha uhitaji; naye hakusita kunihudumia kama mpenzi wake. Aliomba kunioa. Alikuja kwa ndugu zangu na kujitambulisha kiutaratibu kabisa. Hapo, mipango ya ndoa ilianza. Nilitaka kujifanyia sherehe ya kuagwa ila mwishoni kabisa Pharao akasimamishwa kazi na kufungiwa akaunti zake zote za benki. Pesa yangu na michango ya harusi kutoka kwa baadhi ya watu wangu wa karibu nilimkabidhi Pharao. Lengo lilikuwa ndoa ifanyike kwa mafanikio na ifane. Mipango yote ilienda sawa. Siku kumi kabla ya ndoa Pharao alipata tatizo lililohitaji pesa ya dharura, kwakuwa akili iliwaza ndoa tu sikukumbuka kuhusu vitega uchumi alivyonidanganya kuwa anamiliki.


**RIWAYA: NGUVU YA KIAPO**

Inapatikana katika kitabu (nakala ngumu) na soft copy (nakala tepe) kwa bei ya kirafiki.

**KITABU** - Tsh 10,000
**Dar es salaam:**

- Duka la Kona ya Riwaya - 0655428085
- Kalamu Tulivu Magomeni - 0718975659
- Posta Mpya kwa Joji - 0713454152
- Temeke kwa Eva Mrema - 0742630141

Soft Copy (Nakala tepe) PDF - Tsh 5,000
'Offer' kupitia Ngurumo ya Mwandishi ni - Tsh 3,000
Lipa kwa **MPESA LIPA NAMBA 36499709 Eva John Mrema**

# RIWAYA: NGUVU YA KIAPO (07) - Na: Eva Mrema

Niliomba mkopo wa dharura na siku nne kabla ya ndoa nilimpatia kiasi cha shilingi milioni kumi. Ukiongeza na pesa za mchango shilingi za kitanzania milioni nane, tayari nilimpatia milioni kumi na nane. Sijui kama nililogwa au ni karma ya maisha yangu kabla ya haya ila nilimkopea mume wangu mtarajiwa pesa kwa kuweka rehani nyumba yangu. Maandalizi yaliendelea kwa kasi ya ajabu. Tuliwasiliana kadri tulivyoweza. Ndoa tulikubaliana ifungwe Babati, kwani ndugu zake wengi waliishi huko pia. Mimi nilisafirisha ndugu kutoka Tanga alikozaliwa mama na mashangazi wachache kutoka kusini. Nilialika jamaa kutoka Arusha ambako wazazi wangu waliishi kwa kipindi kirefu sana cha uhai wao. Marafiki kutoka sehemu mbali mbali nao niliwaalika" Machozi yalianza kunitiririka na hapo Sunche akanisogelea na kunikumbatia. Nilijituliza kisha nikaendelea.

"Asubuhi ya siku ya ndoa Pharao hakuwa akipatikana kwenye simu. Sikujishughulisha sana na hilo. Nilizingatia kupendeza maana ilikuwa siku kubwa zaidi maishani mwangu. Nilikwenda saluni na marafiki zangu. Tulipendezeshwa haswaa!
Nilijigharamikia kila kitu kwakuwa niliijua hali ya dharura iliyomkumba Pharao. Si kwamba sikuwaambia marafiki zangu tu juu ya hilo, hata ndugu na jamaa sikuwapa nafasi ya kuona udhaifu wa mume wangu mtarajiwa. Kila kitu kilionekana kizuri. Nilipendeza na kuvutia machoni pa kila mja. Nilijitazama mara kadhaa na kukubaliana na mkono wa mrembaji. Kazi yake ilijithibitisha bila kujieleza kwa kinywa. Mipango ya uchukuaji wa matukio kwa mfumo wa picha na video uliendelea na kufanya hali iwe ya kufurahisha na kusisimua. Nilipatiwa vitafunwa nikanywa na sharubati ya limao. Baada ya mambo yote mazuri nilivalishwa gauni langu la harusi.

Nilipendeza balaa! Niliingia garini nikisindikizwa na sauti za matarumbeta pamoja na vigelegele. Msafara wenye magari manne ya kifahari, na magari saba ya kawaida ulitembea kwa madoido na honi nyingi zilizopigwa kiufundi sana. Nilifika kanisani na kungojea kwenye gari. Muda wa ndoa ulipangwa kuwa saa kumi kamili alasiri. Hadi saa kumi na moja bwana harusi hakuwa kawasili. Simu yake kuna muda ilipatikana na kuishia kutopokelewa, na kuna muda haikupatikana. Hofu iliniingia. Nilitoka garini na kuingia kanisani. Ibada ilianza hali kila mmoja akinong'ona la kwake. Binafsi uaminifu niliompa Pharao ulitosha kuniambia kama hatokuja kwenye harusi basi kapata ajali njiani.


Wakati ibada ikiendelea aliingia mzee wa kanisa na kumnong'oneza kitu mchungaji. Mchungaji alitangaza ujio wa Pharao, na kunitaka nisogee madhabahuni, tabasamu lilirejea usoni na kwa unyenyekevu mkubwa nikasogea mbele. Dakika mbili zilipita tena, kiasi mchungaji alionesha kukwazika. Niliuona wajihi wake vizuri japo nilivaa shela. Nilisikia mtembeo wa mtu, ni kama watu wote walistaajabu kumuona, nilihisi minong'ono japo nilijizuia kugeuka nyuma. Tayari ilikuwa saa kumi na mbili na dakika hamsini, na aliyeingia hakuwa Pharao. Mwanamke aliyebeba mtoto mgongoni alijongea hadi madhabauni. Alinitazama kwa chuki na mwisho alinizabua kibao. Nilishangaa. Kulikoni! Mwanamke yule aliyeonekana kuchoshwa na maisha yake alimpokonya mchungaji kipaza na kujitambulisha. "Mimi ni mke wa Pharao mnayemngojea hapa.

Tuna ndoa ya miaka mitano na tumejaaliwa watoto wawili. Huyo Pharao si lolote zaidi ya tapeli wa mapenzi na pesa. Hayo ndio maisha yake. Najua katoka kwako na pesa ya kutosha, atatoweka na kurejea nyumbani siku zikiisha. Atapata kichezeo kingine na kukifanyia alivyokufanyia. Wewe ni mwanamke wa tatu kuachwa madhabahunni na Pharao, baada ya kupata alichokihitaji. Hakuna ndoa wala ndoano Pharao ni mume wa mtu na ni tapeli, poleni kwa usumbufu na niwashauri mabinti kabla hamjaletwa kudhalilishwa madhabahuni namna hii, chunguzeni hao wanaume. Siku hizi wenye ndevu zao, wanadanga kuliko wanawake na mbaya zaidi ni kwamba wao wanajua kuwa mna shauku sana na ndoa. Jihadharini. Mchungaji naomba unisamehe" alihitimisha kusema hayo mwanamama yule na kutoa cheti cha ndoa kwenye mkoba wake. kuwekeza wazazi wangu wakati wa uhai wao.

*Itaendelea...*

**BURUDIKA**
www.kitabumarket.co.tz

## Tangazo





www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi

jamvilasimulizi@gmail.com